# Nipashe

Ijumaa Januari 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580468

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Bweni** lililochomwa 2018 laungua tena, wanafunzi mbaroni

UKURASA 3



**Biden** aahidi demokrasia ushirikiano, heshima, utu

UKURASA 19

RIPOTI MAALUM

# Wajawazito wapimwa juu ya meza, uzito wa mtoto kwenye mti

UKURASA 4

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MWALIMU JELA MIAKA 30 KUMBAKA MWANAFUNZI**

MWALIMU wa Shule ya Msingi Isomya, Manispaa ya Singida, Mjengi Samsoni Munkeny...


## Mbunge afariki dunia, JPM amlilia

UKURASA 2



Kinamama wa Kijiji cha Nyagisya, wilayani Tarime, mkoani Mara, wakiwa na watoto wao pamoja na wajawazito, wakihama kutoka kwenye huduma ya kliniki iliyokuwa ikifanyika chini ya mti na kuelekea katika Shule ya Msingi Nyagisya mapema wiki hii, kwa ajili ya kuendelea na huduma hiyo, baada ya kuwapo kwa dalili za mvua. **PICHA: DINNA MANINGO**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Operesheni ya DC yanasa shehena bidhaa za bandia

UKURASA 2


**MICHEZO** **MWAMBUSI AJIWEKA KANDO YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Operesheni ya DC yanasa shehena ya bidhaa bandia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SHEHENA ya vinywaji bandia imenaswa katika moja ya maghala yanayodaiwa kumilikiwa na mfanyabiashara mmoja mkoani Kilimanjaro ikiwa imefichwa katikati ya magunia ya vyakula vya mifugo.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alisema kwa sasa wanaendelea kumhoji mfanyabiashara huyo, mkazi wa Wilaya ya Hai pamoja na dereva wa bodaboda kutokana na tuhuma hizo.

Mfanyabiashara anayedaiwa kukutwa na shehena hiyo iliyokuwa na pombe kali, ametajwa kuwa ni Alex Swai pamoja na dereva wa bodaboda, Fedrick Moshi ambaye pia anashikiliwa kutokana na tuhuma hizo.

Ole Sabaya na kamati ya ulinzi na usalama, maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Polisi na watendaji wa halmashauri hiyo, walifanya operesheni ya kamata kamata saa 8:00 usiku, Januari 20, mwaka huu.

"Hawa watu tayari nimewakabidhi kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) washughulike nao."

"Kinachofanywa na watuhumiwa hao ni wizi na wanadhani serikali imelala, haijalala. Serikali ya Rais John Magufuli inahangaika usiku na mchana kutafuta kodi na ninyi mnakwepa kodi. Mnauza mali hizi usiku tu kwa nini? alihoji Ole Sabaya."

Katika operesheni hiyo, Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Ernest Mhapa, alisema mfanyabiashara huyo aliomba leseni ya kufanya biashara ya rejareja, lakini amekengeuka na kufanya biashara ya jumla muda usiokubalika kisheria.

Timu hiyo iliyoongozwa na Sabaya ilimkamata pia mwendesha bodaboda huyo, anayedaiwa kusambaza bidhaa ambazo zinadaiwa kutolipiwa kodi.

## Mbunge afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MARTHA Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), amefariki dunia India alikokuwa anapatiwa matibabu, uongozi wa Bunge la Tanzania umethibitisha.

Taarifa ilioyotolewa na Idara ya Habari na Elimu ya Bunge jana, ilibainisha kuwa Spika Job Ndugai alitangaza kifo hicho kilichotokea saa saba usiku wa kuamkia jana kwa saa za India katika Hospitali ya HCG Mumbai, India alikokuwa anapatiwa matibabu.

"Nimepokea kwa mstuko na masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa Martha Umbulla. Ninatoa pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, waheshimiwa wabunge na wananchi wa Mkoa wa Manyara.

"Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na subira katika kipindi hiki kigumu," Spika Ndugai alinukuliwa katika taarifa hiyo ya Bunge.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia ya marehemu inaratibu mipango ya mazishi na taarifa zaidi zitaendelea kutolewa.

JPM AMLILIA

Jana, Rais John Magufuli alituma salamu za rambirambi kwa familia ya mbunge huyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli pia amemtumia salamu Spika Ndugai, wabunge wote, wananchi wa Mkoa wa Manyara na wote walioguswa na kifo hicho.

"Mheshimiwa Martha Umbulla alikuwa mpole, mchapakazi na mpenda maendeleo. Ninazikumbuka jitihada zake za uongozi akiwa Mkuu wa Wilaya na akiwa mbunge," alisema.

Aliwaomba wanafamilia kuwa na moyo wa uvumilivu na ustahimilivu katika kipindi kigumu cha majonzi na kumwombea Marehemu Umbulla pumziko jema.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhiwa baadhi ya vitabu vya historia ya Mwalimu Julius Nyerere na Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, baada ya kumaliza mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mwalimu jela miaka 30 kubaka mwanafunzi, kumpa ujauzito

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

MWALIMU wa shule ya msingi Isomya, Manispaa ya Singida, Mjengi Samsoni Munkeny,i amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kutiwa hatiani kwa makosa ya kubaka na kumpa mimba mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo.

Katika shauri la jinai namba 81/2020, Mwendesha Mashtaka, Patricia Mkina, alidai tukio la kwanza la ubakaji, lilitokea kati ya Aprili, 04,mwaka 2019 na Julai,19,mwaka 2019.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mfawidhi wa Wilaya, Aristida Tarimo alisema, kwamba katika kosa la kwanza la kumbaka mwanafunzi huyo, anamhukumu adhabu ya miaka 30 jela, na katika kosa la pili la kumpa mimba anamhukumu kifungo cha miaka miwili jela, na kwamba adhabu zote zitaenda pamoja.

Awali katika shauri la jinai namba 81/2020, Mwendesha Mashtaka, Patricia Mkina, alidai kwamba tukio la kwanza la ubakaji lilitendwa na mshtakiwa kati ya Aprili 04,mwaka 2019 na Julai 19, mwaka 2019.

Aidha, Mkina alidai siku ya tukio mshtakiwa akiwa katika maeneo ya Kijiji cha Isomya, Kata ya Mwankoko, alimbaka mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), mwenye umri wa miaka 16, anayesoma katika Shule ya Msingi Isomya.

Katika shtaka la pili la kumpa mimba mwanafunzi, ilidaiwa na Mwendesha Mashtaka huyo kuwa katika kipindi cha kati ya Aprili 04,mwaka 2019 na Julai,19, mwaka 2019 mshtakiwa huyo baada ya kumbaka alimpa ujauzito mwanafunzi huyo.

Hata hivyo, baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo alikana, na ndipo upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi watano wakati mshtakiwa hakuwa na mashahidi.

Akitoa ushahidi wake, mwanafunzi huyo alidai katika kipindi hicho mara kadhaa wakati akitoka shuleni, mshtakiwa alikuwa akimwelekeza waende vichakani, na walipofika huko alikuwa akimwelekeza kuvua nguo na yeye (mshtakiwa) akivua nguo za kwake.

Mwanafunzi huyo aliieleza mahakama kwamba matukio ya vitendo hivyo yaliendelea hadi Mei, 2019 na ndipo baada ya wazazi wake kuhofia hali aliyokuwanayo waliamua kwenda kumpima, na kugundulika ana ujauzito.

"Baada ya matokeo ya vipimo vya madaktari ndipo wazazi wake walimuuliza kuwa ujauzito huo ni wa nani,ambapo naye alimtaja mwalimu Mjengi Samsoni Munkenyi na ndipo mzazi alipotoa taarifa kwa ofisa mtendaji wa kata, mkuu wa shule na hatimaye kituo cha polisi, ambapo walipatiwa fomu namba tatu (PF3)," alidai Mkina.

**HABARI KITAIFA**

# Bweni laungua, wanafunzi mbaroni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SEHEMU ya bweni la wavulana katika Shule ya Sekondari Mang'oto wilayani Makete mkoani Njombe, imeungua moto na kusababisha hasara.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Veronika Kessy, alitembelea katika shule hiyo jana na kubainisha kuwa bweni hilo pia liliungua kwa kuchomwa moto na mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo mwaka 2018 na ameagiza kuchukuliwa hatua mara moja kwa waliohusika.

"Nilipopokea taarifa za kuungua kwa bweni la Mang'oto, nilipatwa na mfadhaiko kwa sababu bweni hili liliungua mwaka 2018 mwezi wa tatu (Machi) na tukafanya jitihada kubwa kuchangisha wananchi, wadau ili kupata fedha na kurudisha hili bweni sehemu yake. Sasa katika kipindi cha miaka miwili bweni linaungua tena katika mazingira yaleyale," alisema.

Mkuu wa wilaya huyo alisema hatua za awali zimechukuliwa huku akiwataka wanafunzi wanaowafahamu waliofanya kitendo hicho, kutoa ushirikiano kupitia kwa walimu wao.

"Kama kuna mtu mnamfahamu amefanya hicho kitendo, mumfuate mwalimu wa malezi, nenda ukamwambie, itakuweka huru," Kessy alisema.

Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na maofisa wengine wa serikali wamefika katika shule hiyo na hatua za awali ni kupiga kura ili kuwabaini wahusika na baada ya hatua hiyo, kamati hiyo iliondoka na wanafunzi kadhaa kwa ajili mahojiano zaidi.

Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Gift Kyando, aliwataka wanafunzi kutambua wajibu wao wawapo shuleni na siyo kujiingiza katika matukio ya kihalifu.

"Ukasirike vyovyote, lakini siyo kuchoma bweni wala kuchoma darasa, ninyi mmechoma bweni mara ya pili sasa, wazazi wenu huko wanahangaika, wewe unachoma mahala pa kulala," alisema Kyando.

Ofisa Elimu wa kata hiyo, Furaha Kyando, alimteua Mwalimu Jacob Mdibwa kusimamia shule kwa kipindi ambacho uchunguzi unaendelea juu ya tukio hilo.



Mkuu wa Wilaya wa Iringa, Richard Kasesela (kulia), kwa niaba ya serikali akikabidhi watoto mapacha walioungana kwa Sista Grevacia Kindole ambaye ni Mkuu wa Shirika la Masista la Mtakatifu Theresia katika kituo cha kulelea watoto wanye mazingira magumu cha Tosamaganga, wilayani humo, mkoani Iringa jana, kwa ajili ya kupata malezi baada ya wazazi wa watoto kutokuwa na uwezo wa kuwalea. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Jafo aziweka kikaangoni h/shauri kupeleka bil. 2/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amezitaka halmashauri tisa, ambazo hazijatoa asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha Sh. bilioni 2.36, zipeleke fedha hizo ndani ya wiki mbili.

Pia, amewataka wakurugenzi wa halmashauri hizo siku ya Jumatatu kuwasilisha maelezo kwa Katibu Mkuu TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, kujieleza sababu za kutotoa fedha hizo kama ilivyoelekezwa.

Halmashauri, hizo ni ya Kakonko iliyotakiwa kupeleka Sh. 59,768,100, Kigoma Ujiji, Sh. 256,782,035, Halmshauri ya Wilaya ya Uvinza, Sh. 156,160,520, Halmashauri ya mji wa Nanyamba, Sh. 125,798,931.

Nyingine ni Tandahimba Dc, Sh. 295,869,100, Chalinze Dc Sh. 815,645,087, Sumbawanga Dc, Sh. 240,867,200, Madaba Dc, Sh. 74,607,500 na Mbinga Dc, Sh. 344,507,219.

Jafo, alitoa maagizo hayo jana wakati alipokuwa akitoa taarifa ya hali ya ukusanyaji wa mapato ndani ya halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020, jijini hapa.

Alisema katika kipindi hicho halmashauri zilitoa mikopo kiasi cha Sh. bilioni 22.33 kwa makundi hayo ikiwa ni asilimia 35, ya bajeti kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni Sh. bilioni 64.46.

Alisema, uchambuzi wa taarifa unaonyesha kuwa halmashauri 14 zimechangia zaidi asilimia 75 ya bajeti ya mwaka ya mikopo hiyo, na halmashauri 31 zimechangia kati ya asilimia 50 hadi 74 na halmashauri 87, zimechangia kati ya asilimia 20 hadi 49.

"Halmashauri 44, zimechangia chini ya asilimia 20 na halmashauri tisa hazijatoa kiasi chochote, sasa hizi halmashauri tisa zihakikishe ndani ya wiki mbili zinapeleka fedha hizo na Jumatatu wapeleke maelezo kwa Katibu Mkuu wakieleza sababu ya kutotoa fedha hizo, Halmashauri ya Chalinze yenyewe ilishawasilisha maelezo yake," alieleza Jafo.

Aliitaja halmashauri iliyoongoza katika utoaji wa mikopo hiyo kuwa ni Halmashauri ya Musoma ambayo imechangia asilimia 107 ya bajeti ya mikopo hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ikiwa ya mwisho kwa kuchangia asilimia nne.

**HALI YA UKUSANYAJI MAPATO**

Waziri Jafo alisema kwa mwaka wa fedha 2020/2021 halmashauri zilipanga kukusanya Sh. bilioni 814.96 kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani na katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, zilikuwa zimekusanya Sh. bilioni 381.27 sawa na asilimia 47 ya makisio ya mwaka.

Alisema uchambuzi wa taarifa za mapato ya vyanzo vya ndani ya halmashauri katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, umeonyesha kuwapo kwa ongezeko la mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha Sh. bilioni 24.5 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho 2019 sawa na ongezeko la asilimia saba.

**MIKOA KINARA**

Aliitaja mikoa mitano iliyoongoza kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani yaliyokusanywa kwenye mabano kuwa ni Katavi (62%), Manyara (57%), Songwe (56%), Geita (55%) na Njombe (52%).

Mikoa mitano iliyoongoza kwa kigezo cha pato ghafi ambalo ni wingi wa mapato ya ndani yaliyokusanywa ni Dar es Salaam (51%), Dodoma (40%), Mwanza (45%), Mbeya (40%) na Pwani (47%).

**HALMASHAURI ZILIZOONGOZA**

Waziri Jafo alizitaja halmashauri tano zilizoongoza kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani yaliyokusanywa ni Masasi DC (88%), Momba DC (81%), Njombe DC (80%), Hanang DC (75%), Nachingwea DC (73%).

Aidha, halmashauri tano zilizoongoza kwa kigezo cha pato ghafi ambao ni wingi wa mapato ya ndani yaliyokusanywa ni Ilala MC (51%), Kinondoni MC (51%), Dodoma CC (39%), Temeke MC (52%) na Arusha CC (43%)

Jafo, alitaja baadhi ya matatizo yaliyojitokeza katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi hicho kuwa ni baadhi ya halmashauri kutegemea zaidi chanzo cha ushuru wa mazao na hivyo kushindwa kufikia malengo kutokana na kutokulipwa kwa wakati.

Pia, baadhi ya halmashauri kujiwekea makisio kwenye vyanzo ambavyo hazina uhakika wa kukusanya.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO. 207 YA MWAKA 2020

ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ... MDAI

DHIDI

HAULE G. FABIAN ... MDAIWA

KWA: 1. HAULE G. FABIAN
2. NEEMA M. MLOPE

POPOTE ULIPO

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 26.01.2021 saa 7:00 Mchana. Mbele ya mh. RUBOROGA

ANGALIZO:

Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi wa 01, 2021

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

RIPOTI MAALUM

## DARASA LINAPOGEUZWA KLINIKI

# Wajawazito wapimwa juu ya meza, uzito wa mtoto kwenye tawi la mti

**Na Dinna Stephano, TARIME**

NYAGISYA ni kijiji kilichoko katika Kata ya Kiore wilayani Tarime mkoani Mara, ambacho hadi sasa miaka 12 ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), unaelekeza kiwe tayari kimepata zahanati, lakini kukosa kwake kunawapa makali ya maisha wakazi wake.

Kukosekana kwa huduma hiyo, moja ya waathirika wakuu ni wajawazito na watoto ambao wanalo hitaji la lazima, kuanzia kiafya, kijamii pia kisheria chini ya rungu la MMAM.

Hata hivyo, watekelezaji wa mpango huo hawana muda wa kupoteza, wamebuni mpango mbadala chini ya maelekezo ya 'kliniki inayohama', wameteua jengo la shule na miundombinu yake kuwa mahitaji ya kliniki na tayari wanatekeleza majukumu yaleyale kama ya zahanati na kituo cha afya.

Uchunguzi wa Nipashe, unabaini ni hatua mbadala kuwapunguzia wahitaji adha ya kutembea umbali wa kati Km mbili kwenye Zahanati ya Gamasara na Km nne iliko Zahanati ya Mtana, zote ziko kata jirani na hospitali ya wilaya inapatikana umbali wa Km 14. Nauli za huduma pekee ya pikipiki ni kati ya Sh. 3,000 na 5,000.

Vilevile, imegundulika kuwapo migogoro ya wanakijiji hao wanapokwenda kutibiwa katika moja ya zahanati hizo wananyima huduma.

Mpango huo mbadala unazibebesha majukumu meza na viti vya wanafunzi, kuwa sehemu ya mahitaji maalum ya kufanikisha kliniki ya mjamzito, hali kadhalika matawi ya miti iliyo jirani ni mahitaji mardhawa kufanikisha kliniki ya mtoto na vyote vimewezekana.

Kwa vipi? Hapo ndipo Nipashe ikawa shuhuda wa namna MMAM inavyotekelezwa, wakati kiti kikiendelea na wajibu wake wa siku zote, meza inakuwa kitanda maalum cha mjamzito na nje ya darasa.

Vivyo hivyo, kwa mahitaji ya mwana kliniki ambaye ni mtoto, miti iliyo nje ya mazingira ya madarasa ambayo ni mahususi kwa ajili ya maslahi ya mazingira, nayo inapewa matumizi mapya ya kuwa nyenzo sahihi ya kuning'iniza mizani hata uzito wa mtoto ukajulikana kuhitimisha mahitaji ya kliniki.

Katika ufanikishaji wa kliniki hiyo tembezi juzi, Nipashe ilishuhudia mwitikio mkubwa wa wanakijiji cha Nyagisya na huenda wengine toka jirani, kukiwa na mjumuiko mkubwa wa wajawazito na kinamama wenye watoto.

Hata hivyo, ilibainika kwamba madarasa hayo yanatumika muda wa mchana wanafunzi wakiwa wamekwenda kula, wanaohudumiwa na ratiba ya wahudumu wa kliniki watatu, japo siku ya ushuhuda wa gazeti walikuwa na udhuru alikuwapo mmoja.

Katika kuhakikisha kuwa huduma haikosekani kwa mujibu wa ratiba, wakazi hao wameandaa mbadala wa ofisi ya kijiji, ambako kuna godoro maalum walilonunua kwa kuchangishana kuwahudumia.



Huduma ya kliniki ikiendelea darasani katika Shule ya Msingi Nyagisya, baada ya dalili za mvua kusitisha shughuli hiyo, lililokuwa likifanyika chini ya mti. **PICHA : DINNA MANINGO**

Ufafanuzi wa Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyagisya, Ghati John, kwa mwandishi wa gazeti hili ni kwamba sababu za huduma hizo kufanyika mahali hapo ni kutokana na kuwapo mgogoro kati ya kata yao ya Kiore na kata jirani ya Manga.

"Tukiwa hatuna vikao na hakuna watu wengi tunaowahudumia, tunawaachia ofisi wanawahudumia wajawazito.

"Ninawapongeza wananchi kwa kujitolea kuhakikisha tunajenga zahanati, wagonjwa na wajawazito wanateseka sana, uongozi wa kijiji tulikaa na uongozi wa shule tukashauriana eneo likapatikana la kujenga zahanati.

"Ninawaomba wadau mbalimbali waguswe watusaidie tukamilishe ujenzi," alisema.

Kwa mujibu wa MMAM, kila kijiji kinapaswa kuwa na zanahati, kata iwe na kituo cha afya, hali kadhalika hospitali inapatikana wilayani.

Vilevile, mwandishi alithibitishiwa kalenda ya kliniki inayohama kwamba, kijijini Nyagisya inapatikana mara moja kila mwezi, walengwa wakuu wakiwa ni wajawazito na watoto.

### WANAOHUDUMIWA

Furaha Joseph, mkazi wa kijiji hicho, alisema: "Mimi ni mmoja wa kinamama tunaoteseka kuitafuta huduma ya afya, hatuna zahanati.

"Ukiugua au kwenda kupata huduma ya kliniki, mpaka ujipange uwe na nauli Sh. 3,000 ya pikipiki kwenda Mtana na 5,000 kwenda hospitali ya wilaya, kama hauna inabidi utembee kwa miguu, inachosha."

Happiness Johanes, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alitaja adha nyingine ya kuhudhuria zahanati jirani ya Mtana, huwa wanakataliwa na kuelekezwa kwenda Zahanati ya Gamasara au hospitali ya wilaya, akiitaja moja ya shinikizo lililowafanya kudai kliniki tembezi kijijini kwao.

"Tukienda Mtana, wauguzi wanatuambia tunawasumbua, 'mnakuja tu kurundikana hapa', ukiwa unaanza kliniki, wanakwambia uende hospitali ya wilaya.

"Tunashukuru serikali yetu ya kijiji ilikakaa ikaona ni kwanini tuendelee kuteseka, tukaona ni bora huduma ya kliniki tuifanye hapa kwetu hata kama ni chini ya mti, inatusaidia kupunguza umbali na gharama za nauli na kauli mbalimbali za kukatisha tamaa.

"Umeshuhudia mwenyewe kwa macho yako, huwa tunapima hapa chini ya mti, mvua ikinyesha, tunahangaika sehemu ya kupimia na kujikinga.

"Ikinyesha, tunaenda ofisi ya kijiji, nako wakiwa na vikao vyao, tunaondoka tena, tunaenda shuleni, tunaomba tunapewa darasa.

"Lakini sasa hivi wanafunzi wamejaa, hakuna madarasa, inabidi tusubiri wanafunzi wakienda kupata chakula, ndiyo tunaingia, kama hakuna mvua, tunakaa chini ya mti.

"Nesi anafunga kikoi juu ya kenchi, watoto wanapimwa uzito, kwa wajawazito wanaunganisha madawati au juu ya meza, analala anapimwa kuangalia kimo cha mtoto, mlalo, mapigo, kama anacheza, huduma anapata zote isipokuwa uzito na wingi wa damu hatupimwi.

"Ofisi ikiwa wazi, kuna godoro wananchi tulinunua linawekwa chini ya sakafu, mjamzito unalala, nesi anapiga magoti chini anakupima.

"Tukiwa nje, wanaweka meza mjamzito unalala juu ya meza, unapimwa, meza tunaazima shuleni," alibainisha.

Simulizi nyingine ni kutoka kwa Rhobina Meng'anyi, alisema huduma hiyo wanayoipata chini ya mti ni huruma ya serikali ya kijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime baada ya kuona wajawazito na watoto wanateseka kupata huduma.

"Mama mkwe wangu alikufa njiani akiwa anaenda kujifungua, alivuja damu nyingi kutokana na mitikiso ya pikipiki, barabara mbovu halafu umbali mrefu.

"Aliacha watoto sita na mke mwenzangu alipofika hospitali ya wilaya, alijifungua lakini mtoto alifariki dunia alizaliwa akiwa kachoka. Mimi nina watoto sita, wakiugua, ninapata shida sana, hakuna zahanati," alisema.

"Ikiwa usiku gharama ni 30,000 huku ni porini na ni mbali kuna fisi wengi, unakuta unakaa mbali na umelala na mke wako unapigiwa simu wakati mwingine saa saba za usiku au saa nane hali hii inawashinda mabodaboda wengi mwingine akikupigia simu unaacha kupokea na wakati huo mgonjwa ana hali mbaya anakosa msaada anazidiwa anaamua kujifungulia nyumbani wengine wanakufa, au uchungu unazidi anazalia njiani,"alisema Wambura.

### KUTOKA KWA MUUGUZI

Rebeka Samson, muuguzi katika Zahanati ya Mtana, anayetoa huduma ya kliniki chini ya mti kwenye Kijiji cha Nyagiswa, alisema ameamua kutoa huduma hiyo kwa kuwa ni sehemu yake licha ya kukutana na vikwazo vingi wakati wa utoaji huduma.

"Huwa tunakuja wauguzi watatu, leo (juzi) niko mwenyewe, mmoja anaumwa, mwingine yuko masomoni, tunatoa huduma ya kliniki tu kwa watoto na wajawazito inayotolewa mara moja kwa mwezi na tunahudumia wagonjwa zaidi ya 50 kama unavyoona.

"Kwa kuwa niko peke yangu, kila kitu ninafanya mimi, ninapima watoto, wajawazito na huduma ya chanjo," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyagisya, Waitara Kemo, alisema tayari wananchi wamechimba msingi kwa nguvu zao, wamechanga fedha na kusomba mawe na mchanga, matofali 3,500, mifuko 30 ya saruji pamoja na kuchanga Sh. milioni moja, ili kuanza ujenzi wa zahanati.

Nipashe katika kusaka mustakabali wa tatizo hilo, ilihamia kwa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Joseph Ngowi, ambaye alisema hakuwa na taarifa za watoto na wajawazito kupata huduma ya kliniki chini ya mti.

"Sitaruhusu huduma kutolewa chini ya mti, siku zote ofisi yangu ilikuwa inajua huduma inatolewa kwenye majengo ya shule, kama serikali ya kijiji haijajipanga kuandaa jengo kwa ajili ya huduma hiyo, wananchi watalazimika kwenda kuifuata kata jirani ya Manga kupata huduma ya kliniki katika Zahanati ya Mtana," alisema.

Ngowi alisema huo ni mwongozo wa serikali kwenye huduma na watumishi wanalifahamu hilo na kwamba muuguzi aliyetoa huduma chini ya mti, amefanya makosa.

# TAKUKURU yageukia katika ubadhirifu fedha za miradi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi, imesema kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, inatarajia kuongeza nguvu katika uchunguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa huo kutokana na malalamiko ya ubadhirifu wa fedha unaofanywa na baadhi ya watumishi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Oktoba - Desemba 2020, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Katavi, Faustine Maijo, alisema fedha nyingi zinazotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali, hutumika vibaya na kupelekea miradi hiyo kutokamilika au kujengwa chini ya kiwango.

Alisema mbali na miradi ya maendeleo, pia wataongeza nguvu kufuatilia ubadhirifu wa fedha katika vyama vya ushirika, mikopo umiza kwa wananchi na watumishi wa umma, fedha za ruzuku kwa wanafunzi ambazo zinatumiwa vibaya na walimu wakuu au wasimamizi wa fedha hizo.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema katika kipindi cha Oktoba-Desemba mwaka jana, taasisi hiyo imefanikiwa kuokoa Sh. milioni 170.396, kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo Mpate Saccos, Idara ya Misitu, chama cha ushirika, Kasekese Amcos na ukusanyaji wa ushuru.

Alisema wanaendelea na uchunguzi wa watumishi wa idara ya afya watatu wa Kituo cha Afya Ilembo wanaokabiliwa na tuhuma za wizi wa dawa za serikali, kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika kituo hicho.

Alisema TAKUKURU Mkoa wa Katavi pia imefanikiwa kumrejeshea Sh. 23,000 Hadija Mkumbo ambayo alitapeliwa na mmoja wa wauguzi wa hospital ya mkoa huo, Lugata Mazuka, baada ya mgonjwa huyo kupata ajali maeneo ya Kalema na kupelekwa katika hospitali hiyo kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza baada ya kupokea fedha, Hadija alisema aliambiwa achangie pesa kwa ajili ya kifaa cha x-ray kilichoharibika, na alipotoa, alipewa rufani ya kwenda kutibiwa Hospitali ya Mbeya yeye pamoja na majeruhi wengine na kuambiwa wachangie pesa ya nauli akasema hana pesa hivyo, ataenda kwa usafiri wake na baada ya kurudi, aliomba pesa zake Sh. 23,000 akajibiwa pesa haipo, wameitumia.

# TRA yaonya wafanyabiashara wasiotumia EFD

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, imewataka wafanyabiashara wote wilayani humo kuendelea kutumia mashine za kielektroni za kutolea risiti (EFD) pamoja na wanunuzi kuomba risiti hizo wanaponunua bidhaa.

Akizungumza na gazeti hili jana ofisini kwake Meneja wa TRA wilaya ya Bunda, Dickison Xamara, alisema wafanyabiashara wote wanatakiwa kuwa na mashine hizo na kuzitumia kwa kutoa risiti halali kwa wateja wao kwa kuwa ni kosa kisheria kutotoa risiti.

Xamara alisema ni kosa pia kwa mnunuzi kutokudai risiti na mfanyabiashara yeyote asiyekuwa na mashine hizo au kutokutoa risiti akibainika atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kupigwa faini pamoja na mnunuzi pia.

Hata hivyo, aliwapongeza wafanyabiashara wanaolipa kodi ya serikali kwa wakati kwa kuonyesha ushirikiano mzuri kwa mamlaka hiyo.

"Natumia fursa hii kuwashukuru wafanyabiashara ambao ni waaminifu na wamekuwa wakitoa kodi kwa wakati kwa kuwa kodi wanayotoa ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wote wakiwamo wao wenyewe," alisema.

Alisema kwa kipindi cha miezi sita iliyopita mamlaka hiyo imefanikiwa kukusanya mapato mengi zaidi ya Shilingi bilioni moja na kuvuka lengo lililokuwa limewekwa.

"Na Rais wetu Dk. John Magufuli mara kwa mara amekuwa akihimiza watu kuendelea kulipa kodi, hivyo ninawaomba wafanyabiashara wote waendelee kutoa kodi kwani ni kwa ajili ya manufaa yetu sote, ikiwamo kununua madawa, kulipa mishahara ya watumishi, kujenga miundombinu na mambo kadha wa kadha ya kimendeleo," alisema Xamara.

Baadhi ya wafanyabiashara hao akiwamo Salumu Yahaya wa mjini Bunda, walisema kuwa TRA imekuwa ikiwapatia huduma nzuri, ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu ya ulipaji wa kodi na manufaa yake na umuhimu wa kutumia mashine za EFD.

"Kodi tunayolipa ni kwa ajili ya manufaa yetu ya kimaendeleo hivyo ninawaomba wafanyabiashara wenzangu tuendelee kulipa kodi, tusifanye ujanja ujanja katika suala hilo," alisema Salumu.

Katika hatua nyingine Xamara alisema zoezi la Namba ya mlipakodi (TIN) kwa watumishi wa serikali katika wilaya hiyo limekwenda vizuri.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikagua shamba la mkonge la Kigombe lililopo chini ya kampuni ya Amboni Plantation Ltd, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. Wa pili kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa shamba hilo, Casbert Nail na kulia ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa Tanga, Henry Shekifu. **PICHA: OWM**

# Mkakati waja kusaidia wenye VVU kuendelea kutumia dawa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKA la AGPAHI linalojihusisha na utoaji wa huduma kwa watu waliopata maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU), limeanzisha mkakati wa kuhakikisha watu wanaotumia dawa za kufubaza VVU wanaendelea kuzitumia.

Meneja miradi wa shirika hilo mkoani Shinyanga, Dk. Adarick Makome, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kutahmini miaka minne ya mradi wa boresha, ambao umelenga kutoa huduma kwenye afue za VVU na Ukimwi ili kuhakikisha maambukizi yanapungua.

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2016, na sasa unaelekea ukingoni, hivyo wameona ni bora wafanye tathmini ya miaka minne iliyopita ili kubaini changamoto zilizojitokeza na kuzifanyia kazi na kufikia malengo waliyojiwekea.

"Vipaumbele ambavyo tumeviweka wakati tukielekea kuhitimisha mradi wetu ni kuhakikisha wateja wote ambao wanatumia dawa za kufubaza makali ya VVU wanabaki kwenye huduma na kutumia dawa hizo,"alisema Makome.

"Vipaumbele vingine ni kuboresha huduma kwenye vituo vya kutolea huduma kwa waathirika wa VVU, maabara za kuchukulia sampuli za watu ambao wanajitokeza kupima, pamoja na kuimarisha maeneo ya huduma ya masuala ya ukatili wa kijinsia (GBV), kwenye huduma za afya," aliongeza.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk, Yudas Ndugile, alisema hali ya maambukizi ya VVU mkoani humo ni asilimia 5.9, huku akishukuru shirika hilo kuendelea kushirikiana na serikali katika mapambano ya kupunguza maambukizi mapya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Viongozi kwa hili la shule Dar mbadilike*

**WAKATI** huu viongozi wa Dar es Salaam, wakiwamo mkuu wa mkoa na wengine kadhaa wanatafuta njia zote na kujituma kwa kila namna kufanikisha ujenzi wa madarasa ya sekondari King'ong'o ambayo wanafunzi wanakaa chini kutokana na kukosa madawati.

Lakini pia, wengine wanasongamana kwenye vyumba vya madarasa kwa sababu hawana madarasa ya kutosha.

Kwa kuzingatia maelekezo ya Rais John Magufuli, watendaji na viongozi wanafanya juhudi zote kukamilisha ujenzi huo, jambo ambalo limepata msukumo baada ya kuonywa na Rais kuwa kama hawatafanikisha jukumu hilo, waanze kutafakari njia zao.

Rais anachozungumzia hapa ni uwajibikaji na si kufanyakazi kwa utaratibu huo wa zima moto.

Viongozi kuwa karibu na wananchi ili kuhamasisha, kuanzisha na kusimamia miradi na shughuli za maendeleo ni jambo muhimu.

Kwa kutumia maelekezo ya Rais, anayowapa watumishi na viongozi mkoani Dar es Salaam, watendaji na wakuu wengine sehemu nyingine wabadilike.

Suala la madawati lipo. Ni sugu, viongozi walipatie ufumbuzi wa kudumu. Si hivyo, changamoto ya madarasa haijawahi kumalizika. Ni suala linalohitaji ufumbuzi ili ufanikishaji wake uwe endelevu. Haipendezi kila mara kusubiri mpaka Rais azungumze, inaonekana kuwa viongozi wamepumzika na wanafanyakazi kwa mazoea.

Pamoja na changamoto za ukosefu wa madarasa, madawati na mabweni, vyoo shuleni ni changamoto.

Mara nyingi viongozi wanashindwa kusimamia uchimbaji wa mashimo na kujenga vyoo vya kisasa kwa ajili ya wanafunzi wetu. Tusijisahau huu ndiyo wakati wa kuwajibika na kuendesha shule kwa ujasiriamali.

Ni vyema viongozi wa mkoa na wilaya wakafikiria kuendesha shule kijasiriamali kwa kuanzisha migahawa na maduka ya kuuza bidhaa za wanafunzi ili fedha zinazopatikana zitumiwe kwa maendeleo ya shule.

Kwa mfano shule ziwe na maduka ya kushona sare, kuanzia suruali, mashati, sketi, sweta na soksi kwa ajili ya wanafunzi wake.

Kadhalika ziwekeze kwenye kuuza , daftari, kalamu, mifuko, karatasi , utoaji wa huduma za kuchapisha na kurudufisha nakala mbalimbali na fedha zinazopatikana ziingie kwenye mfuko wa shule.

Kadhalika wanafunzi wengi ni wateja wa vyakula, vinywaji na vitafunwa, kwa hiyo pengine ndiyo fursa kwa shule kufikiria utaratibu wa kuanzisha migahawa ya kupika na kuuza vyakula.

Tunaamini kuwa yote hayo yatawezekana iwapo kutakuwa na kamati za mapato na uchumi zinazolenga kufanikisha upatikanaji wa pesa za kuinua uchumi wa shule pamoja na kukuza uwekezaji.

Usimamizi wa biashara hasa za sare siyo mgumu kwa vile idadi ya wanafunzi inafahamika na hivyo mapato yao yanafuatiliwa kwa utaratibu unaojulikana.

Ni wazi wakati umefika kwa walimu, kamati kwa shule za msingi na bodi kwa zile za sekondari kubadilika na kuanza ujasiriamali.

Imekuwa ni kawaida kuendesha shule, hospitali na taasisi nyingine nyingi za umma kwa mazoea bila kuwa na mabadiliko wala mbinu za utafutaji na ujasiriamali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# *Tunapomiliki ardhi tuwe na busara ya miliki na matumizi*

**MARA** zote kanuni na pengine sheria, zinaelekeza kuwa mtu anapomiliki radhi kwa namna yoyote anakutana na wajibu wa ulazima kwamba akifanyie matumizi yanayostahili, akioanisha na makusudi ya kumiliki ardhi.

Inapokuwa mtu anashindwa kuendeleza sehemu hiyo ya ardhi, kuna maana kwamba tayari kuna vikwazo, isipokuwa kuna makusudi maalum.

Wapo wanaochukua ardhi, huku wakijua hawana uwezo au dhamira ya kuendeleza na inabaki hatua wanaweka vibarua walima tu na baadhi yanayishia kuwa pori.

Kama ardhi inachukuliwa na haiendelezwi, mwisho wa siku inakuwa pori, hali inayosababisha hata kuwapo mazingira ya athari kama vibaka na wadudu au wanyama wenye madhara katika eneo hilo

Nasema, kama mtu unachukua ardhi na anashindwa kupaendeleza, basi ardhi ajue hiyo inatakiwa awape wenye uhitaji na uwezo wa kuitumia, kwa ajili ya kujinufaisha kwa kipato.

Mtazamo huo ndio uliofikiwa na uongozi wa kitongoji Cha Marogoro kilichopo Mkuranga, kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaomiliki ardhi na wanashindwa kuiendelea.

Dai la uongozi huo ni kwamba mtazamo wa kushindwa kuendeleza ardhi hiyo, inasababisha wanyama wakali kujificha na hata watu wasiojulikana nao kujificha kwa ajili ya kufanya mabaya wanayonuia, ni ardhi inayogeuka eneo hatari.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Marogoro Mjini, Abdull Hilary, aliiambia Nipashe kwamba:

> **Mwenyekiti wa Kitongoji cha Marogoro Mjini, Abdull Hilary, aliiambia Nipashe kwamba: "Mashamba hayo kutokana na kutoendelezwa kwa muda mrefu, yamekuwa ni pori na hali hiyo inakuwa atari kutokana na kuwapo uwezekano wa kukaa wanyama wakali, nyoka na hata kujificha watu wasiojulikana ambao wanaweza kupafanya hifadhi,"**

"Mashamba hayo kutokana na kutoendelezwa kwa muda mrefu, yamekuwa ni pori na hali hiyo inakuwa atari kutokana na kuwapo uwezekano wa kukaa wanyama wakali, nyoka na hata kujificha watu wasiojulikana ambao wanaweza kupafanya hifadhi,"

Mwenyekiti huyo anasema, msingi wa kanuni walio nayo kiuongozi ni kwamba kila anayeamua kumiliki ardhi, maana yake ni kwamba anakusudia kuifanyia kazi inayostahili na si kupatelekeza.

Anasema, kuna watu wanaojitambua kwamba wanajua wamechukuwa mashamba kwa kipindi kirefu na wameshindwa kuyaendeleza jambo ambalo si sahihi, hivyo kinachopaswa sasa ni kuyaendeleza na kama wakinshindwa kukamilisha hilo, basi uongozi wa kijiji utaingilia kati kuchukua hatua stahiki.

"Kama mtu anachukua shamba na anashindwa kuliendeleza, anakuwa kafanya makosa na anatakiwa aliendeleze," anasema.

Pia, inaelezwa kwa asilimia kubwa wanaochukua shamba ni wakazi wa nje ya Mkuranga, ambao wengi wanakosa utubutu wa walau kutembelea maeneo yao kuona jinsi namna yalivyoharibika na kuwa pori.

Anasema kama mtu anatokea kuchukua eneo la shamba na anashindwa kuliendeleza, basi busara binafsi ni kumpatia mwingine mwenye uhitaji anayepaweza

na baadae akijipanga atalichukuwa eneo lake na kuliendeleza.

Hilary anasema, taarifa ya wahusika wameshazitoa na atakayeshindwa kuyatekeleza aliyoambiwa hatua kali za kisheria, zitachukuliwa

# TMDA yaandaa maabara bora

**Na Devota Mwachang'a,**

MWANZA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeanza maandalizi ya kuifanya Maabara ya Kanda ya Ziwa kuwa maabara bora na maalum kwa uchunguzi wa dawa za kuua viini vya bakteria (vipukusi).

Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa, Sophia Mziray, alisema jana kuwa kwa sasa maabara ya Kanda ya Ziwa ndiyo pekee kwa nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) yenye uwezo wa kupima vipukusi ikiwamo vitakasa mikono (sanitizers).

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea maabara hiyo jijini Mwanza kuona namna inavyoendesha shughuli zake, Mziray alisema ni maabara ya pekee kwa kanda mzima yenye kutoa majibu yasiyo na shaka.

"Maabara hii ipo kwenye taratibu za kufanywa kuwa maabara kubwa ya kisasa, bora na bobezi ya kupima vipukusi katika Afrika, hasa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema Mziray.

Alibainisha kuwa maandalizi ya kuwa na wachunguzi wabobezi yameanza na yapo katika hatua nzuri, pia nyaraka zimeandaliwa, upembuzi yakinifu umefanyika ili kujiridhisha kama rasilimali zinatosheleza kuwa maabara bora zaidi.

"Kwa kuwa ni maabara pekee katika Kanda ya Ziwa, tunaendelea kuchunguza dawa kutoka kanda nyingine, kutoa elimu kwa umma, na kuhakikisha Watanzania wanapata bidhaa bora, salama na zenye ufanisi.

" Alibainisha kuwa maabara hiyo ina mifumo ambayo imethibitishwa ili kuhakikisha ubora wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi unaendelea kuwapo, akisema wanatumia mfumo wa ufuatiliaji na udhibiti wa dawa sokoni (PMS).

Alisema bado kuna kikwazo cha udhibiti wa bidhaa kwenye Kanda ya Ziwa, mipaka ya Mutukula, Sirari, Kyerwa na pia Bandari ya Mwanza South na Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa kuwa dawa hizo huvushwa kwa njia zisizo halali.

# 60 wanaodaiwa 'madada poa' mbaroni

**Na Ibrahim Joseph,** DODODMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma linawashikilia watu 60, wanaodaiwa kuwa ni 'madada poa' pamoja na wateja wao kwa kosa la kufanyabiashara ya kuuza miili yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, , alisema jana kuwa jeshi hilo liliendesha msako wa kuwakamata watu hao juzi usiku na kuwakamata watu hao eneo la Air Port jijini Dodoma.

Muroto alisema jeshi hilo lilifanikiwa kuwakamata madada poa 42, katika mtaa huo na wateja wao 18, ambao ni wanaume wanaodaiwa kufanya nao biashara hiyo kwenye madanguro mawili yaliyopo mtaa huo.

Hata hivyo, Kamanda Muroto hakutaka kutaja majina ya watuhumiwa hao na kudai kuwa watafikishwa mahakamani haraka ili kujibu mashtaka yanayowakabili ya kufanya biashara hiyo haramu ya kuuza miili yao.

Kadhalika, alisema katika msako huo jeshi hilo liliwakamata watu wawili wanaodaiwa kuwa ni wamiliki wa madanguro hayo yanayotumiwa na madada poa hao kufanya biashara hiyo haramu.

"Watu wote hawa watafikishwa mahakamani wakati wowote ili kujibu tuhuma za kufanyabiashara ya kuuza miili yao na wengine kumiliki madanguro na wanaume waliokamatwa wataunganishwa kwenye kesi hiyo hiyo," Muroto.

Wakati huo huo, alisema jeshi hilo lilifanya operesheni ya kuwakamata waendesha bodaboda na bajaji wanaodaiwa kuvunja sheria za usalama barabarani.



Mkurugenzi wa Baraza la Mchele Tanzania (RCT), Winnie Bashagi, akiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzalisha mchele bora wenye viwango vinavyokidhi ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi kwa wasindikaji wa bidhaa hiyo, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Watano wapandishwa kizimbani kwa tuhuma za uhujumu uchumi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WATU watano wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Singida, wakikabiliwa na tuhuma mbali mbali ikiwemo uhujumu uchumi.

Kesi hiyo inawahusu watu watatu, akiwemo Joachimu Albogasti (35) mkazi wa Kijiji cha Mwanduigembe, wilayani Iramba, Samweli Filemoni(35) mkazi wa Kijiji cha Ilongero na Abdulkaid Mwamba (52).

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Petrida Muta alidai kuwa katika shitaka la kwanza la kuharibu miundombinu ya serikali, ilidaiwa kuwa Disemba 31,mwaka jana kwa nyakati tofauti washitakiwa waliingilia miundombinu ya vifaa vya umeme vya Kampuni ya CCCE ETERN CONSORTIUM.

Katika shitaka la pili la kukutwa na mali zinazodhaniwa kuwa za wizi, Mwanasheria wa Serikali Benedict Colle alidai kuwa Disemba 31 mwaka jana washitakiwa hao walikutwa na mali inayodhaniwa kuwa ya wizi yenye thamani ya Sh 2,430,970.

Baada ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Singida, Evod Kisoka kuwasomea mashitaka, washitakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na Mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Mwanasheria wa Serikali alisema Mahakama hiyo inasubiri kibali kutoka kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali ili kuendelea na kesi hiyo na kwamba washitakiwa wote wamepelekwa rumande baada ya kushindwa kutekeleza masharti ya dhamana hadi Februari 02,mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa tena.

Wakati huo huo, wakazi wawili wa Mjiji Singida, Monko Msaghaa (27) pamoja na Juma Mohamed Mungwabi (38), wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Singida wakikabiliwa na tuhuma za wizi.

Ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Almachus Bagenda kwamba Disemba 25 hadi Disemba 29 mwaka jana asubuhi katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Monko Msaghaa aliiba lita moja ya mafuta ya Transfoma yenye thamani ya Sh 10,000.

Katika shitaka la pili la wizi, Bagenda alidai kwamba Disema 25 hadi Disemba 29 mwaka jana asubuhi, Juma Mohamed Mungwabi aliiba nusu lita ya mafuta ya Transfoma yenye thamani ya Sh 5,000.

Baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa wa Singida, Elimo Masawe kuwasomea mashtaka washitakiwa walikana na wote wako rumande baada ya kushindwa kutekeleza masharti ya dhamana hadi Februari 04, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa tena.

# Asasi za kiraia zatengewa bil. 10/-

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Foundation for Civil Society (FCS) imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya Asasi za Kiraia (CSO's) zilizopo nchini 150.

Lengo la fedha hizo ni kwa ajili ya kufanikisha utendaji kazi wa asasi hizo kufanya shughuli za maendeleo kwa wananchi.

Meneja Mipango wa FCS, Francis Uhadi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwa waandishi wa habari katika mkutano uliohudhuriwa pia na wawakilishi wa asasi hizo kutoka maeneo tofauti ya nchi.

Alisema pia mafanikio ya FCS kwa mwaka jana, ilifanikisha kutoa kiasi cha fedha Kama hicho kwa asasi 150, ilisaidia kukuza ujuzi kwa viongozi wa kisiasa husan wabunge na madiwani.

"Lengo letu ni kukuza uelewa wa jamii hususan katika shughuli za maendeleo, " alieleza Uhadi.

Kadhalika, Uhadi alisema uelewa mdogo kwa jamii kuhusu masuala tofauti ni kati ya matatizo ambayo yanasababisha kutofahamu haki zao za ushiriki katika shughuli za kimaendeleo.

Meneja Mipango huyo, alisema kwa upande wa Zanzibar na Mwanza, kumerekodiwa matukio mengi ya watoto kuwadhalilisha hivyo juhudi ziongezwe

Uhadi alisema FCS itaendelea kushirikiana na serikali, kuhakikisha watoto na masuala ya Kijinsia yanazingatiwa ili kuondokana na udhalilishaji au ukatili.

Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi, Tathmini, Utafiti na Mafunzo, Gestad Haule, alisema urasimu bado ni tatizo kwa baadhi ya taasisi za umma.

"Bado tunahitaji elimu kwa umma kuwajengea uwezo, ili wafahamu haki zao," alisema Haule.

Emannuel Simon, Mratibu wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB), alisema tangu mwaka 2016, asasi yake umekuwa ikinufaika na ruzuku kutoka FCS.

Alisema serikali iharakishe kuchapisha vitabu vitakavyowalenga vipofu na wenye uoni hafifu.

"Nchi yetu iliingia na kusaini mkataba wa Marrakesh Treaty, sisi tunauliza mchakato wa vitabu kuchapishwa kwa ajili ya vipofu na uoni hafifu," alisema Simon. Katibu wa asasi ya Action for Justice in Society (ASISO), Tatu Mrutu, kuna mwitikio chanya kwa jamii kuripoti matukio yanayohusiana na udhalilishaji katika maeneo ya wilaya ya Mwanga mkoani, Kilimanjaro.

Alisema hali hiyo imefanya matukio ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto kushuka kutokana na jamii kuwa na uelewa.

Mrutu aliongeza kwamba matukio kama hayo yanayotokea watu hutoa taarifa vituo vya Polisi haraka kwa hatua zaidi.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto (kushoto), akizungumza na waendesha bodaboda nje ya kituo cha kikosi cha usalama barabarani, jijini Dodoma jana, baada ya kuendesha msako wa kuwakamata wavunja sheria za usalama barabarani. Kushoto kwake ni Mkuu wa kikosi cha usalama barabarani wa mkoa huo, Boniface Mbao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hapi aagiza polisi kukamata wazazi wanaotumikisha wanafunzi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amepiga marufuku wazazi mkoani hapa kuwatumikisha wanafunzi mashambani badala ya kwenda shule huku akiagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wazazi wote watakaobainika kufanya hivyo.

Alitoa agizo hilo jana wakati akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa na madawati katika shule za Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

Alisema, wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari na wenye sifa ya kuanza elimu ya msingi wanapaswa kuripoti shule kuanza masomo badala ya kutumikishwa shughuli za shamba na biashara ndogo ndogo.

Aliwataka wazazi wote kupeleka watoto wao shule na watakaoshindwa kufanya hivyo watawajibika kisheria kwa kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Pia, alipiga marufuku walimu wakuu kuwachangisha wanafunzi michango kinyume na utaratibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, uliotolewa kwa walimu wa shule zote nchini.

"Wapo baadhi ya walimu wamekuwa na tabia ya kuwaagiza wanafunzi kuleta fedha za masomo ya ziada, natangaza hapa leo ni marufuku kwa walimu kuwaagiza watoto fedha hizo, atakayekiuka atawajibika," alisema Hapi.

Katika hatua nyingine , ameagiza halmashauri zote za Mkoa wa Iringa kuhakikisha zinakagua na kuyakarabati madawati mabovu, pia kushughulikia suala la upungufu wa vyumba vya madarasa kwa halmashauri zenye changamoto ya vyumba hivyo.

Msitahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema Manispaa ya Iringa imeendelea kutekeleza agizo la Waziri Mkuu la vyumba vya madarasa na kuwa hadi sasa wanafunzi wote wamefanikiwa kuanza masomo. Alisema suala la upungufu wa madawati linafanyiwa kazi na kupitia mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) anayewakilisha mkoa huo, Salim Abri Asas, amejitolea madawati 500 kusaidia kupunguza tatizo hilo.

## RC aagiza ukaguzi kubaini wanaovaa hirizi shuleni

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amewaagiza walimu wakuu na wakuu wa shule kuwakagua wanafunzi ili kubaini iwapo wanavaa hirizi wawapo shuleni, ili kukabiliana na vitendo vya kishirikina.

Agizo hilo alilitoa jana kwenye mkutano alioufanya Kijiji cha Malonje wilayani Sumbawanga kutokana na baadhi ya wananchi kudaiwa kuwa na tabia ya kuwaita waganga wa jadi, maarufu lambalamba, na kuwalipa fedha ili wawasafishie nyumba na mali zao.

"Kutokana na baadhi ya wazazi wa wanafunzi kuamini ushirikina kupita kiasi, huenda wakawapa hata watoto wao hirizi na matunguli ili waende nayo shuleni wakiamini kuwa vitu hivyo vitawalinda watoto wao hali ambayo itasababisha usumbufu kwa wanafunzi wengine.

"Walimu wakuu na wakuu wa shule, wakagueni wanafunzi wenu ili muone kama wamevaa hirizi, kwani hayo ndiyo yanayowasumbua wanafunzi wengine, utakuta kwenye shule wanafunzi wanaugua ugonjwa wa kuanguka ovyo, hirizi ndiyo inasababisha hali hiyo," aliagiza.

Mkuu wa mkoa alisema haiwezekani serikali ikawa inaongoza watu ambao wanaishi kwa kuamini ushirikina, hivyo aliwapiga marufuku waganga hao wa jadi kufanya shughuli zao mkoani humo. Wangabo pia aliliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka waganga hao wa jadi nyumba hadi nyumba, kijiji hadi kijiji na kuwakamata kisha kuwachukulia hatua za kisheria kutokana na kutapeli wananchi kwa kisingizio kuwa wao ni waganga na watatatua shida zao.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Halfan Haule, alisema shida kubwa ni wananchi wenyewe wamekuwa wakichangishana fedha hata baadhi yao kufikia hatua ya kuuza mali zao ikiwamo mifugo ili wapate fedha ya kuwalipa waganga hao wafike kijijini kwao kusafisha miji yao na kuondoa mikosi.

# Walimu wakuu hawajui kiasi fedha za ruzuku kwa wanafunzi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya walimu wakuu wa shule za msingi wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, hawajui kabisa kiasi sahihi cha fedha ambacho serikali inatoa kama ruzuku kwa kila mwanafunzi katika shule zao.

Hali hiyo imebainika katika utafiti uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali la Kaeso, linalotekeleza mradi wa ufuatiliaji Rasilimali za Umma katika Sekta ya Elimu (PETS) kwa kata za Zimba, Kapenta na Miangalua kwa ufadhili wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Mratibu wa mradi huo, Ayoub Mlengo, alisema jana wakati akiwasilisha taarifa ya utafiti huo kwenye kikao cha wadau wa sekta ya elimu kilichofanyika katika ukumbi Samazi uliopo mji mdogo wa Laela wilayani humo.

Alisema utafiti huo uliwalenga walimu wakuu 14 wa shule za msingi za kata hizo, ambapo tisa kati yao sawa na asilimia 56 walisema hawajui kiasi ambacho kila mwanafunzi anapaswa kupata kama ruzuku, huku asilimia 43.8 ndio wenye uelewa wa fedha anayotakiwa kupata kila mwanafunzi.

" Walimu wakuu wana uelewa tofauti tofauti kuhusu ruzuku ya serikali katika shule za msingi. Wapo wanaosema ruzuku ya mwanafunzi ni Sh. 12,000 kwa mwaka, wengine ni kuanzia Sh. 7,500 hadi 10,000 wakati wapo wasiojua kabisa," alisisitiza

Alisema kutokuwa na uelewa wa kutosha wa miongozo inayotolewa na wizara husika ndio sababu kubwa ya walimu hao kutofahamu fedha ambayo kila mwanafunzi anapaswa kupata.

Akichangia mada katika kikao hicho, Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga, Patricia Mpewa, alisema kila mwanafunzi anatakiwa kupata Sh. 10,000 ambapo asilimia 40 inapelekwa kununulia vitabu na 60 unafanya matumizi mengine kama vifaa vya mitihani na ukarabati.

Alisema pia kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya shule kupokea fedha kidogo ukilinganisha na wanafunzi waliopo, na kwamba hali hiyo inatokana na wanafunzi wengi kutosajiliwa katika mfumo wa wizara ya elimu.

"Walimu wakuu wanafanya uzembe kusajili wanafunzi katika mfumo ndio maana wanakosa fedha za ruzuku..... serikali inapeleka ruzuku shuleni kutokana na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kwenye mfumo.

Diwani wa Kapenta, Fredrick Simon Magazi, alisema mradi wa ufuatiliaji rasilimali za umma katika sekta ya elimu umesaidia kubaini madudu yaliyofichika, na kwamba kuna kikundi cha watu katika kata hiyo kilifanya ubadhirifu na umebainika.

Alisema ubadhirifu huo ni kuuza mabati18 na mbao 80 zilizotolewa na mbunge wa zamani wa jimbo la Kwela kwa Shule ya Msingi Ngomeni, hivyo kuahidi kufuatilia hadi zipatikane.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati (mwenye kipaza sauti), akizungumza na walimu na wananchi wa Usinge, baada ya kukagua madarasa katika Shule ya Sekondari Usinge, wilayani Kaliua, jana. **PICHA: TIGANYA VINCENT.**

# Uzalishaji mbegu bora mkonge kuongezeka

**Na Ashton Balaigwa,TANGA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), inakusudia kuzalisha mbegu bora ya mkonge kutoka miche milioni 2.5 ya sasa inayozalishwa kwa njia ya vikonyo kufikia milioni 10 kwa mwaka itakayozalishwa kwa njia ya chupa.

Hatua hiyo ni baada ya kuifanyia ukarabati maabara yao iliyopo katika Kituo cha TARI Mlingano mkoani Tanga.

Uzalishaji huo unalenga kukidhi mahitaji ya soko la dunia la mkonge taklibani tani 500,000 kwa mwaka wakati uzalishaji kwa sasa ni tani 280,000, huku Tanzania ikiwa ya pili kwa uzalishaji huo ikizalisha wastani wa tani 40,000 kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na fursa iliyopo ya uzalishaji.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema uzalishaji wa mbegu bora za mkonge unafanywa kwa kutumia vikonyo ambao unazalisha miche milioni 2.5 kwa mwaka hivyo maabara ya Tissue Culture itakapofanyiwa ukarabati wa kina itaongeza na kufikia milioni 10, hivyo kukidhi mahitaji ya mbegu wa wakulima wa mikoa yote inayolima mkonge.

"Tunataka kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, na hapa tunapozungumza tumeshapanda shamba lenye hekta 31.2 ambapo kuna miche taklibani 2.5 lakini tunataka kuongeza, uzalishaji kwa kutumia maabara baada ya kuifanyia ukarabati mkubwa.

Alisema maabara hiyo inazalisha miche bora taklibani 120,000, lakini ikipanuliwa itaongeza upatikanaji wa mbegu na kufikia miche milioni 10 kwa njia ya chupa kwa mwaka.

Dk. Mkamilo alisema mahitaji ya sasa ya mbegu ya mkonge kwa wakulima wadogo ni miche kati ya milioni 1.2 hadi milioni 1.6, huku wakulima wakubwa wakihitaji miche kati ya milioni 10 mpaka milioni 12.

Alisema kuwa Tanzania ina eneo la hekta 44,123,561 sawa na asilimia 47 linalofaa kwa kilimo cha mkonge wakati eneo linalolimwa ni hekta 64,029.73 sawa na asilimia 0.2 hivyo endapo uzalishaji wa mbegu kwa kutumia maabara utafanikiwa, utasaidia kuongeza uzalishaji wa mkonge.

# Watakiwa kutunza vyanzo vya maji

**Na Frank Kaundui, MOROGORO**

WAKAZI wa Manspaa ya Morogoro wametakiwa kutunza mazingira pamoja na kulinda vyanzo vyote vya maji ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji uliopo kwenye baadhi ya maeneo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (MORUWASA), Mhandisi Tamim Katakweba, ambapo alisema serikali imedhamiria kuondoa changamoto ya maji, hivyo vyanzo vyake vilindwe.

"Morogoro tunakabiliwa na changamoto ya maji mbali na kuwa tuna mito mingi ambayo pia hutegemewa na mikoa ya jirani, hali hii yote inasababishwa na uharibifu mkubwa ma vyanzo vya maji maeneo mbalimbali ya mkoa,"alisema Katakweba.

Alisema mbali na jitihada za serikali kuhakikisha tatizo la maji katika mkoa huu linapatiwa suluhisho la kudumu ili wananchi waweze kupata maji ya uhakika, pia kila mtu anao wajibu mkubwa wa kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinalindwa.

Mhandisi Katakweba alisema serikali inafanya kazi kubwa kukakikisha wananchi wa mkoa huo wanapata maji salama na yenye uhakika, na kwamba kutokana na juhudi hizo, kuna miradi ya maji mbalimbali inayoendelea kutekelezwa.

"Serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maji hususani hapa Manispaa, hivyo ili kufanikisha hili, ni wajibu wetu sote kulinda vyanzo vyote vya maji,"alisema Katakweba.

Alisema kuwa wapo watu wanaoishi maeneo ya milimani ambao wamekuwa wakiharibu miundombinu ya mito ambayo ndiyo tegemeo la vyanzo vya maji katika mkoa huu na kusababisha baadhi ya maeneo kukosa maji kwa uhakika.

Aliitaja baadhi ya miradi ya maji katika Manispaa ya Morogoro kuwa ni wa Madadu unaoghalimu Sh. bilioni 1.7, Mindu bilioni 2.9 na Kihonda bilioni 3.5 na Bigwa unaoghalimu Sh. bilioni 2.4.

Fatuma Omary, mkazi wa Kihonda, alisema mtaa wake unakabiliwa na changamoto ya maji hali inayowalazimu wananchi kununua dumu la lita 20 kwa Sh.500 hadi 700, hivyo miradi hiyo ni neema kubwa kwao.

# Wanaonyonya maziwa ya wake zao waonywa

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wanaume walio na imani kwamba kunyonya matiti ya wake zao wanaonyonyesha kunawaondolea uchovu wa pombe 'hang over', wametakiwa kuondokana na dhana hiyo kwa sababu ni chanzo cha udumavu wa watoto.

Vitendo hivyo vinatajwa kujitokeza kwa baadhi ya mikoa ikiwamo Shinyanga na Iringa.

Mkurugenzi wa Afya, Lishe na Maendeleo ya Jamii Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, alibainisha hayo alipozungumza na Nipashe, kuhusu suala hilo na kufafanua kuwa kitendo hicho kinachofanya na baadhi ya wanaume kwa wake zao, kinafifisha lishe ya mtoto pamoja na ukuaji

"Kitendo hicho kinachelewesha ukuaji wa mtoto hususan wanaonyonyeshwa walio chini ya miaka mitano, jamii iondokane na dhana hiyo, na kuwaacha watoto wakue ipasavyo," alisema Dk. Kapologwe.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti hivi karibuni, baadhi ya familia zilizohojiwa kutoka mikoa hiyo, walikiri kufanya hivyo na kwamba hunyonya maziwa ya wake zao kwa zamu na mtoto.

"Hakuna tatizo ninaporejea nyumbani, nilikwambia mke wangu mahitaji nikate pombe, mtoto anaweza akasubiri, au mimi nikaanza mtoto akasubiri," alisema mmoja wa mwanamume ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake, katika mahojiano na kituo kimoja cha redio.

Mke wa mwanamume huyo, alisema alihisi mume wake alipata taarifa za kunyonya matiti ili kupata maziwa katika mazungumzo ya mtaani na kuwenda kuzifanyika kazi nyumbani.

"Nahisi mwenzangu huyu alisikia mtaani, nafikiri akataka apate uhakika yeye mwenyewe. Mganga Mkuu wa Halmashauri Mkoa Shinyanga, Dk. Mamrita Bashike, katika mahojiano na redio hiyo, alisema kuna tatizo hilo, na kwamba wahudumu ngazi ya jamii wanapotembelea wajawazito huwashawishi waume zao kuhudhuria kliniki ili kupewa elimu.

"Wanapofika zahanati mhudumu wa afya anatoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama wanaonyonyesha na waume zao wakiwapo, ili kufahamu namna ya kumpa haki mtoto ya kunyonya bila kuwathiri watoto," alisema Dk. Bashike.

Dk. David Nicholas alisema kitendo hicho ni kuwadhulumu watoto haki yao ya mwili na kukua ipasavyo.

Kwa kipindi tofauti taasisi za lishe zimekuwa zikisema kitendo hicho kimechangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa watoto wenye udumavu na kukosa lishe bora, na kwamba zaidi asilimia 47 ya watoto mkoani Iringa wana udumavu.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Horticultural Association (TAHA), Jaqueline Mkindi, wakati wa mkutano wa wadau wa zao la mkonge uliofunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa jijini Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Mbunge aibua sakata la kupotea gari la h/shauri

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

MBUNGE wa Rorya mkoani Mara, Jafari Chege (CCM), ameibua madai kuwa gari la Halmashauri ya Rorya aina ya Land Cruiser V8 lenye thamani ya Sh. milioni 108 lililonunuliwa mwaka 2007 lilipotea katika mazingira ya kutatanisha.

Mbunge huyo pia ametaka ufanyike uchunguzi wa kina kuhusu suala hilo.

Akizungumza sakata hilo, Chege alisema gari hilo lilinunuliwa na Halmashauri ya Rorya kutoka Kampuni ya Toyota, na kwamba lilipotea tangu kununuliwa na haijulikani lilipo.

Aliomba vyombo vya dola kuanzisha uchunguzi wa kina ili kubaini baada ya kununuliwa lilipotelea wapi kwa kuwa halionekani Rorya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Charles Chacha, akizungumzia sakata hilo mbele ya kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, alisema hajui gari hilo lipo wapi mpaka sasa.

Akitoa ufafanuzi kuhusu sakata la gari hiyo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo wakati huo, Charles Ochele, alisema gari lenye namba SM 6675 aina ya Land Cruiser V8 ilipokelewa ikiwa na namba za STK.

Alisema walipohoji kwenye Baraza la Madiwani kwa nini gari hilo lilipelekwa likiwa na namba za STK, Mkurugenzi alijibu kuwa walichukua namba hizo kutoka TAMISEMI kwa ajili ya kulisafirisha gari hilo kutoka Dar es Salaam kwenda Rorya wakisubiria namba zake halisi za SM.

## NMB yajitosa zao la mkonge

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

BENKI ya NMB imesema itahakikisha inaendelea kutoa huduma za kifedha kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kufufua zao la mkonge na kuboresha uchumi wa wakulima wa zao hilo nchini.

Hatua hiyo inakuja baada ya serikali kuanza mikakati ya kuhakikisha zao hilo linafufuliwa na kuwanufaisha wakulima na taifa kwa ujumla kama ambavyo ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Akizungumza mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa kikao cha wadau wa mkonge kilichofanyika juzi mkoani Tanga, Ofisa Mkuu wa wateja binafsi na biashara wa Benki hiyo, Filbert Mponzi, alisema NMB itaendeleza jitihada za kufufua zao hilo ambazo imezianza.

Alisema kuwa tangu serikali imeanza kulifufua zao hilo, benki hiyo imekuwa ikitoa ushirikiano ambapo imetoa zaidi ya Sh. bilioni 1 kwa ajili ya ununuzi wa matrekta 11 na trela 22 vifaa ambavyo vitapunguza gharama ya uendeshaji na kuongeza tija na pato la wakulima wadogo wa mkonge.


Aliongeza kuwa benki hiyo imeendelea kutoa mikopo ya pembejeo na uendelezaji wa mashamba ya mkonge kwa wakulima wadogo, kati na wakubwa ili kuongeza uzalishaji na mapato ambapo zaidi ya Sh. bilioni 6 zimeshatolewa kwa wakulima wa mkonge.

Alisema NMB imefanikisha kufungua akaunti kwa wakulima zaidi ya 1,500 ambapo akaunti hizo zinajumuisha wakulima mmoja mmoja na wale wanaozalisha kupitia Vyama vya msingi.

" Uwapo wa akaunti hizi unajenga utamaduni wa wakulima kutumia huduma za benki kwa usalama wa fedha zao na mazingira sahihi katika kupata huduma zaidi ya kifedha ikiwamo mikopo," alisema Mponzi.




Mtaalamu aliyebuni uchochoro kwa mchimbaji Laizer hadi kuwa bilionea




Inda, tamaa, upendeleo ni maadui




Liparamba penye tembo wakimbizi, simba weupe na miti inayogeuka jiwe



DK. KALEMANI ZIARANI...

# Watumiao laki tisa nishati kila siku mgodi mdogo watabasamu

• Awaambia 'mambo safi' suala la wakati tu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu katika migodi mbalimbali mkoani Shinyanga, wamekuwa wakitumia gharama kubwa kuzalisha madini hayo kutokana na ukosefu wa nishati ya umeme kwenye migodi hiyo.

Mbadala ambao wamekuwa wakiutumia ni pamoja na mafuta mazito ya kuendesha mitambo ya kufua umeme ili wazalishe madini, pia jenereta zinaziotumia mafuta ya kawaida.

Vyote kwa kiasi kikubwa wanavilalamikia kuwagharimu fedha nyingi.

Mchimbaji mdogo wa madini dhahabu katika mgodi wa Nyangalata uliopo Msalala wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, Alex Manyama, analalamika gharama kubwa za uzalishaji madini, katika wanaposaga mawe yenye dhahabu hadi kufika Sh. 900,000 kwa siku au wastani wa Sh. milioni 19 kwa mwezi

"Kuna wachimbaji wenzangu ambao wana mitambo mikubwa wanatumia zaidi ya kiasi hiki cha pesa ambacho nimekitaja mimi," anasema Manyama.

"Ziara hii ya Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani hapa mgodini, sisi kama wachimbaji wadogo wa madini tunatarajia makubwa kwake ya kupata huduma ya umeme, hivyo tumejawa na matumaini sasa umeme utakuja hapa mgodini, sababu amekuja Waziri mwenyewe na hawezi kutudanganya," anaongeza.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipozungumza na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu katika machimbo ya Nyangalata, wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

Ni aina ya malalamiko yaliyokwishatolewa na Meneja wa Kampuni ya Uchimbaji Madini Dhahabu StamiGold, iliyopo wilayani Biharamulo Mkoa wa Kagera, Mhandisi Gilay Shamika, Desemba mwaka jana, alipokuwa kwenye Maonyesho ya Biashara na Teknolojia ya Madini mjini Shinyanga.

Alitaja gharama wanazotumia kununua mafuta mazito kuendeshea mitambo yao kila mwezi kuzalisha dhahabu, pia jenereta ni Sh. bilioni 1.2, akitoa matarajio kwamba wangetumia nishati umeme, ingewagharimu Sh. milioni 300 kwa mwezi, sawa na robo ya gharama ya sasa.

### WAZIRI NISHATI

Akiwa ziarani katika machimbo ya mkoani Shinyanga, Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani, anasema Rais Dk. John Magufuli, ameshatoa fedha za kuwaunganishia wananchi huduma ya umeme, ikiwamo maeneo yote ya migodi, ili kuongezea kasi ya uzalishaji.

Anasema, sehemu ya mkakati kitaifa kuwakuza wachimbaji wadogo, ili wachimbe kwa ufanisi pamoja na kupanua wigo wa mapato yao, wakiwa ndani ya gridi ya taifa.

Kwa mujibu wa waziri huyo, tafsiri moja ya kutumia umeme wa gridi ya taifa, ni kwamba itaokoa zaidi ya asilimia 80 ya fedha walizotumia awali kuzalisha madini hayo, kupitia matumizi ya mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ya kufua umeme na jenereta.

"Nimefanya ziara kwenye mgodi huu mdogo wa uchimbaji madini uliopo hapa Nyangalata wilayani Kahama, nimejionea mwenyewe namna wachimbaji hawa wanavyoingia gharama kubwa ya kuzalisha madini. Ni kutokana na kutumia mafuta mazito kuendeshea mitambo ya kufua umeme au jenereta," anasema Dk. Kalemani.

Anaendelea: "Wengine wanatumia hadi Sh. milioni 800 kwa mwezi...naliagiza shirika la umeme (TANESCO) walete huduma ya umeme kwenye mgodi huu haraka sana, pamoja na kusambaza umeme kwenye migodi mingine ambayo haina nishati ya umeme, ili waongeza kasi ya uzalishaji madini na kuinua kiuchumi na serikali tupate mapato mengi."

### MBUNGE WA MSALALA

Mbunge wa Jimbo la Msalala, wilayani Kahama, Iddi Kassim, eneo lenye migodi mingi ya dhahabu ukiwamo Nyangalata, anasema tangu zama za kampeni yake alianika kilio cha kupatikana nishati ya umeme migodini, na ziara hiyo ya Waziri wa Nishati, Dk. Kalemani, ni ishara ya faraja jimboni kwake, kilio kufanyiwa kazi.

"Nishati ya umeme itakapofika kwenye maeneo ya migodi hii midogo ya uchimbaji madini ya dhahabu, itaongeza kasi ya uzalishaji madini, kwa sababu wachimbaji wataongezeka, kutokana na wengine walikuwa wakishindwa kumudu gharama za kununua mitambo ya kufua umeme ya mafuta mazito.

"Pia umeme utakapofika kwenye migodi hii, hata shughuli nyingine za kiuchumi zitaongezeka, sababu watafungua vitega uchumi vya kuwaingizia kipato nje na madini ikiwamo kufungua saluni za kike na kiume," anaongeza.

BIASHARA

MJUE FAUSTUS RUTAHINDURWA;

# Mtaalamu aliyebuni uchochoro kwa mchimbaji Laizer hadi kuwa bilionea

• Miaka 28 Mirerani tangu mahafali • Ikitajwa tanzanite, yeye ni 'kila kitu' • Apewa tuzo ya Mjiolojia Bora nchini

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

TANZANITE ni madini yanayopatikana pekee nchini, katika eneo la mgodi wa dhahabu wa Mirerani mkoani Arusha, ikiwa sehemu ya utajiri nyeti ya rasilimali ya asili kitaifa.

Pia, kuna utajiri mwingine wa asili kama dhahabu inayopatikana katika mikoa mama ya Kanda ya Ziwa, kama Simiyu, Shinyanga, Geita na Mara.

Simulizi ya kuibuliwa utajiri wa madini Tanzanite, pia dhahabu mahali hapo na kuibuka mchimbaji mdogo kuweka historia kuwa bilionea, ni zao la ujuzi, ubunifu na usimamizi wa karibu sana kutoka kwa mjiolojia, Faustus Rutahindurwa,

Mkongwe huyo ndani ya Mirerani tangu kuhitimu masomo ya shahada miongo mitatu iliyopita, alipata faragha na Nipashe, akiwa na mengi ya kusimulia na yamejaa msisimko.



Mchimbaji madini wa Mirerani Arusha, Saniniu Laizer, akiwa na madini yaliyomuibua kuwa bilionea, ikiwa ni matunda ya utaalamu na usimamizi wa mjiolojia, Faustus Rutahindurwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### ALIVYOTUA MIRERANI

Rutahindurwa anaanza kwa kujitambulisha: "Taaluma yangu ni mjiolojia. Ni Mtanzania wa kwanza kupata elimu nzuri ya utafiti wa madini ya tanzanite. Nilipata digrii yangu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na nilihitimu mwaka 1992,hivyo kwa miaka 28 hadi 2020 nilikuwa Mirerani."

Anasema akiwa Mirerani alijishughulisha na uchimbaji madini ya grafeti na tanzanite na kabla ya jukumu hilo, aliajiriwa na kampuni ya kigeni ya Samagisi, akiwa mjiolojia wa utafiti wa madini hayo.

Rutahindurwa, anaeleza baadaye kampuni hiyo ilibadilishwa jina na kuitwa Grafeti Tanzania, ikichimba madini ya grafeti, yeye akibobea kuitafiti sehemu ndogo ya madini tanzanite.

Anasimulia mwaka 2000, alihamia kampuni mpya kutoka Afrika Kusini iliyoitwa Tanzanite One, iliyojikita zaidi kuchimba madini ya tanzanite, wakati huo akieleza eneo la Mirerani kijiolojia halikufahamika vizuri sana.

Anasema, kulikuwapo wachimbaji wadogo waliokosa uelewa wa kina na walichimba na kitaalamu, uchimbaji wao ulikuwa na madhara ya kuzamisha mgodi au kufukiwa vifusi vya mchanga, baadhi yao wakipoteza maisha.

Rutahindurwa anataja chanzo kikuu cha ajali kutokea katika mashimo ya uzalishaji, kilikuwa matumizi ya vifaa duni, zikiwamo anachokiita Moko, pia wachimbaji wakitawaliwa na mikwaruzano yao wenyewe.

> **"Niliamua kuacha mshahara wangu mzuri na kwenda kuwashauri wachimbaji wadogo ambao walikuwa wakinihitaji niwasaidie kufanya utafiti.**

Anasema katika mwanzo wa kutumikia kampuni ya mpya ya Tanzanite One, aliungana na wajiolojia wengine kutoka Afrika Kusini kutafiti undani wa dhahabu hiyo ardhini na mzizi wa madini tanzanite ilivyokaaa ardhini.

Mjiololijia huyo anaeleza, alifanya kazi ya kuchoronga mashimo ya kina kirefu chini ya ardhi na kisha walitoa sampuli inayowawezesha kuelewa vizuri jiolojia ilivyokaa, hata wakachora ramani ya mgodi, hatua iliyowawezesha kupata mafanikio makubwa.

Mjiolojia Rutahindurwan anaeleza, katika uongozi wake wa jopo la wajiolojia wenzake waliokiwa wakifanya utafiti, walianzisha migodi tisa ya dhahabu mahali hapo.

### UAMUZI MGUMU

Hata hivyo, mtaalamu huyo anasema uchimbaji ndani ya migodi Mirerani, aliamua kuacha kazi kwenye kampuni hiyo kutokana na wachimbaji wadogo waliohitaji kumtumia ushauri wake.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (kulia), akimkabidhi tuzo Mjiolojia Faustus Rutahindurwa,kutokana na umahiri wa kazi yake, iliyotolewa na Chama cha Wanajiolojia nchini, jijini Mwanza.

Katika hilo aliingia mkataba nao kwa malipo anayoyataja 'kiduchu' ikiwa ni ya asilimia ya wanachopata na aliwasaidia kutafiti wanakochimba na kuwapa stadi ya kugundua yanakopatikana dhahabu.

"Niliamua kuacha mshahara wangu mzuri na kwenda kuwashauri wachimbaji wadogo ambao walikuwa wakinihitaji niwasaidie kufanya utafiti. Niliingia mkataba nao, ingawa malipo ni 'kiduchu'lakini navumilia tu kuwasaidia.

"Hata utajiri wa (Saniniu)Laizer kuwa bilionea (Sh. bilioni 1.7) umetokana na mimi mjiolojia wa Utafiti wa Madini. Baada ya kufanya utafiti wa eneo la kuchimba ambalo nilimshauri kuchimba kilomita mbili kwenda chini ya ardhi, baadaye alipata dhahabu," anaeleza Rutahindurwa.

Anasema utafiti wake ndio kiini cha mafanikio yenye umaarufu mkubwa, Laizer akipata dhahabu aliyoiuzia serikali na baadaye akapewa tuzo ya mchimbaji bora wa dhahabu Mererani na binfasi akitunukia tuzo ya ujiolojia bora nchini.

Rutahindurwa, anasimulia kwamba wakati aliyemuongoza Bilionea Laizer katika uchimbaji huo, pia aliiongoza kampuni nyingine ya Afrika Tanzanite kuchimba dhahabu kitaalamu.

### MAFANIKIO NA MAGUMU

Mjiolojia huyo anaweka wazi magumu ya kufanikisha malengo hayo kikazi, hasa kwa wachimbaji inaangukia kwenye ukosefu wa mitaji ya kuendeshea shughuli hizo, vifaa duni na hasa mitambo inayokidhi mahitaji ya kiufundi.

Pia, ana sura ya pili katika mafanikio kwamba amepiga hatua ya kuanzisha mgodi wake wa dhahabu Mirerani na utafiti wake ndio uliomuibua bilionea Laizer anayevuma kidunia.

Sasa mjiolojia Rutahindurwa, anatoa wito kwa wajiolojia wengine kuhakikisha wanajitahidi kusambaza elimu kwa wachimbaji wadogo, badala ya kujikweza baada ya mafanikio kikazi.

Pia, anaiomba serikiali kuwasaidia wachimbaji wadogo kuwawezesha kupata mitambo ya kuleta tija katika uchimbaji dhahabu.

Rutahindurwa, anawaelekezea ombi wajiolojia kijana kuanza kufanya kazi kwa vitendo kupitia taasisi za madini wanakoajiriwa, ili wapate uzoefu wa awali wanapotoka vyuoni.

"Wanzie kwenye kampuni ili wapate kwanza uzoefu, ndipo waende kufanya utafiti wa madini. Wasijione wao ndiyo 'matawi ya juu' kutumia elimu ya darasani hata kama wana digrii," anasisitiza Rutahindurwa.

### DARASA LA WAKALA

Hidaya Hassani, ni wakala wa jiolojia nchini, anayesema amekuwa akifanya utafiti wa madini tangu walipoanza kazi hiyo mwaka 2005.

Anafafanua majukumu ya wakala wake, akifananisha na alichokisema, kukifanya na kukishauri mjiolojia Rutahindurwa, kwamba wanatoa taarifa za kwanza za utafiti kujua miamba laini, migumu na tabaka zilizopo chini ya ardhi.

Wakala huyo anasema, taarifa hizo huwa wanaziuza kwa kampuni za uchimbaji, pia wachimbaji wadogo madini, ambako wana dira ndefu ya kuwaendeleza kufika mbali, ili waweze kuchimba kitaalami,

Katika kufanikisha hilo Wakala Hadija, anasema wananuia kuongeza taarifa zaidi za kijiolojia, kutembelea waliko wachimbaji wadogo na kuwasaidia kujua kuchimba bora kupitia wataalam na wakala wa jiolojia.

Hata hivyo, anakiri azma hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya uelewa mdogo kutoka kwa wachimbaji wadogo, wakiwa na elimu duni.


Lingine analitaja ni wachimbaji wadogo kuwa na hofu ya kutaifishwa, hata wakaficha taarifa chanya zenye sura ya mafanikio kikazi, haswa ikizingatiwa wengi hawana leseni za uchimbaji madini.



Namna ilivyo kazi ya wachimbaji wadogo wakizama mgodini Mirerani. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Inda, tamaa, upendeleo ni maadui




AKIZUNGUMZA mwaka juzi kwenye hafla maalumu ya kuzindua Ligi Kuu ya Soka kwa wana Yanga 'kubwa kuliko' iliyofanyika Dar es Salaam, Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alielezea kile alichokiona kama si upendeleo, basi ni uzembe kwa baadhi ya viongozi.

Rais Kikwete aliwalenga viongozi wa soka nchini, ambao aliamini kwa kujisahau na kutotimiza wajibu na majukumu yao barabara, walijikuta wakipendelea baadhi ya timu na kuzikandamiza zingine, na kusahau kwamba kwa kuwa wao ni viongozi wa kitaifa na viongozi wa wote.

Ingawa hakutaja majina, lakini walioelewa walielewa alikuwa akilenga kina nani zaidi. Huo ulikuwa ujumbe pia kwa viongozi wengine, ambao ama kwa maslahi binafsi, au uzembe au ujinga, wamekuwa hawatimizi wajibu wao kwa haki na uhakika.

Mifano ipo mingi na dhahiri; mathalan hivi karibuni, Msajiliwa Vyama vya Michezo nchini, alitangaza kufungiwa kwa miaka miwili aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Mbeya, Elias Mwanjala kujihusisha na michezo, kwa kukiuka sheria.

Mwanjala anadaiwa aligombea nafasi hiyo, hata baada ya kumaliza mihula yake miwili kwa mujibu wa Katiba ya Shirikisho la Vyama vya Soka Tanzania (TFF).

Ingawa TFF ilikuwa inajua kosa lililofanyika,



**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

bado haikuchukua hatua, mpaka Msajili alipoingilia kati na kuamua kwa kuzingatia Katiba. Je, kulikuwapo haja gani mpaka ngazi ya juu kuchukua hatua wakati ya chini ikijua tatizo ni nini?

Hivi karibuni, kukawapo taarifa, pia dhidi ya mchezaji wa klabu ya Simba, Benard Morrison, kwamba alitoa ishara chafu, tabia isiyokubalika kwa jamii.

Tuhuma ya ishara kama hiyo ilipata kutolewa huko nyuma na mchezaji Athumani Iddi 'Chuji' na aliadhibiwa.

Si Simba wala TFF iliyotangaza tukio hilo, wala kujibu malalamiko ya watu achilia mbali kuchukua hatua na mambo yanaendelea kimya kimya, ingawa kuna ofisa mwandamizi wa TFF aliulizwa na wanahabari, akajibu wanasikilizia kwanza Simba itafanya nini.

Hiyo nayo kama si upendeleo wa chombo chenye dhamana kwa mchezaji au klabu na uzembe au kutojua wajibu na dhamana, ni nini?

Hivi karibuni wilayani Kinondoni, Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, aliendesha operesheni iliyobaini watu wanaodhalilisha wenye ulemavu, kwa kuwatumikisha kuomba mitaani.

Nderiananga ambaye pia ni mwenye ulemavu, aliteuliwa hivi karibuni na Rais Dk. John Magufuli, lakini ameibua uozo huo siku chache tu baada ya kuapishwa. Je Kinondoni hakukuwapo viongozi?

Inashangaza kuwa mambo yote hayo yalikuwa yakitokea, licha ya gazeti moja nchini kupata kuripoti kwa kina mwaka 2018, lakini ripoti yake ikagonga masikio na macho mfu.

Tafsiri iliyopo hapo ni kwamba, viongozi waliokuwapo walipuuzia taarifa hizo na hivyo kutojishughulisha au wakinufaika na mradi huo uliokuwa dhidi ya maslahi ya Watanzania wanyonge. Walidanganyika kirahisi na wachumia tumbo na kuingia katika biashara hiyo.

Mifano hii inathibitisha ukweli kwamba baadhi ya viongozi wamekuwa hawaisaidi inchi, kwani wanashindwa kuchukua hatua za kukabiliana na adha kama hizo, mpaka mwenye ulemavu mwenzao alipohisi uchungu wao.

Ni bahati mbaya sana, kuwa mpaka katika muhula huu wa pili wa Rais Dk. John Magufuli, bado wapo viongozi hawatendi mpaka wamwone mkuu huyo kafika katika maeneo yao! Alamsiki!

BIASHARA

PORI AKIBA LIPARAMBA

# Penye tembo wakimbizi, simba weupe na miti inayogeuka jiwe

- Maajabu ya maji yanayounda mchora wa ramani Afrika
- Ndege wa kilo 16, kumchinja kibali maalum serikalini



Mfano wa ramani ya Afrika iliyochorwa kwa maji juu ya mwamba, ndani ya Hifadhi ya Liparamba. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

**Na Gideon Mwakanosya,** MBINGA

KATIKA utaalamu na mfumo wa mbuga, pia hifadhi za wanyamapori, ni chache zilizobahatika kuwa na maingilio au mapitio ya wanyama ambayo yana jina mahsusi, ushoroba, kutoka nchi moja kwenda nyingine jirani.

Pori la wanyamapori Liparamba lililopo wilayani Nyasa mkoa wa Ruvuma, ni miongoni imo katika orodha ya mapori au mbuga za wanyama zilizobahatika na hilo.

Ofisa Utalii wa pori hilo, Maajabu Mbogo, anasema lilianzishwa mwaka 2000 na hadi sasa lina wanyamapori wakubwa na wadogo, wakiwamo tembo, simba, chui, viboko, mamba, tandala, pofu, palapala, kuro, nyati, pundamilia, fisi na mbweha.

Mbogo anaeleza kuwa, katika pori hilo kuna aina mbalimbali za ndege kama vile kanga, mbawala na fundichuma.

"Neno Liparamba ni la kabila la kimatengo ambao ni wenyeji wanaoishi wilaya ya Mbinga. Maana ya Liparamba, ni mbuzimawe," anasema Mbogo na kuendelea:

"Pori hili lina makundi makubwa ya tembo, ambao ni wakimbizi, kwa sababu huwa wanatoka Msumbiji na kuhamia Liparamba."

> **Neno Liparamba ni la kabila la kimatengo ambao ni wenyeji wanaoishi wilaya ya Mbinga. Maana ya Liparamba, ni mbuzimawe.**

Anasema makundi makubwa ya tembo wanaotoka Msumbiji, huanza kuingia kwa wingi katika pori la Liparamba kuanzia mwezi Machi wanakoendesha maisha kwa wastani wa miezi minne na kisha Julai, tembo wanaanza safari ya kurudi Msumbiji.

Mbogo anasema, katika ya mwezi Septemba na Oktoba ya mwaka, mahali hapo panabakiwa na tembo wachache sana. Anaendelea na kufafanua:

"Inapotokea kule nchini Msumbiji majangili yamewashambulia tembo au kuwasumbua, tembo hao wanapoingia katika hifadhi ya Liparamba hawatoki. Wanaweza ndani ya pori la Liparamba kati ya miaka miwili hadi mitatu bila kutoka kurudi Msumbiji, kwa sababu Liparamba ni sehemu salama ya kuishi tembo."

Ofisa Utalii huyo anataja maajabu mengine yaliyopo Liparamba, kwamba kumeshawahi kuonekana simba mweupe na analitetea hilo kuwa si jambo geni au la ajabu mahali hapo.

Anavitaja vivutio vingine vilivyopo Liparamba, ni aina mbalimbali za nyoka kama vile jamii ya mamba na kobra, maporomoko ya maji ya Nakatuta katika Mto Ruvuma, ambayo ni kivutio cha asili cha utalii.

### MAAJABU&MTI JIWE

Kwa mujibu wa Ofisa Utalii huyo, ni pori lenye vivutio vinavyofaa kufanya utalii wa kupanda kwenye mawe, ikizingatiwa yapo mengi makubwa na yanafaa kwa utalii wa aina hiyo.

Pia, anataja ndani ya pori hilo kuna utajiri wa miti, akitaja aina ya mtetereka, ambao ukikauka unabadilika kuwa jiwe na na inapatikana kwa wingi katika eneo la Nakatuta, kando ya Mto Ruvuma, kivutio kinachowateka watalii wengi wapenzi watafiti wa miti na mimea.

Mbogo anasema, katika eneo la Nakatuta, pia kuna miti mingine jamii ya kamba ambayo inapokatika, hutoa maji yanayonyweka, mithili ya maji kutoka vyanzo vingine na kukata kiu.

Ofisa Utalii huyo anasema, katika pori hilo kuna mito inayovutia, Mto Lumeme unaomwaga maji katika Mto Ruvuma na kuna mto usiokauka uitwao Lumeme na unaofaa kwa utalii wa kuogelea na kuvua samaki.

Analitaja eneo lingine linalofaa kwa utalii porini humo, ni makutano kati ya Mto Ruvuma na Mto Namakunguru, kwenye jiwe kubwa lenye urefu wa mita 70 kutoka chini ya Mto Ruvuma hadi juu, linalofaa kwa utalii wa kupanda.

Eneo la Mkuyu ndani ya Pori la Liparamba, kuna kivutio kinachowashangaza wengi na maji yanayotiririka kwenye Mto Mkuyu, yametengeneza mfano wa ramani ya Afrika juu ya mwamba.

"Maji yameweza kutengeneza mfano wa ramani ya Afrika juu ya mwamba. Ukichukua ramani ya Afrika na kuangalia ramani iliyotengezwa na maji, hakuna tofauti ni ramani kabisa ya Afrika, haya ni moja ya maajabu katika pori la Liparamba," anasema.

### HUDUMA YA MGENI

Mhifadhi Msaidizi wa pori hilo, Paul Protas, anasema kila mgeni anapofika katika pori la Akiba Liparamba, anaweza kupata nafasi ya kutembelea Bwawa la Mkuyu ambako mtalii anapata nafasi kuogelea na kufanya utalii wa kuvua samaki na kumrudisha ndani ya maji.

Protasi anakitaja kivutio kingine ndani ya pori hilo, ni kuwapo wa ndege aina ya koribustard (Mbawala), ambaye nchini anatumika kama alama ya Taifa.

"Huyu ni ndege mkubwa ana uwezo wa kufikisha uzito kilo 16, ana urefu wa sentimeta 1330. Huyo ni ndege wa kitaifa, anachinjwa kwa kibali kinachoombwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," anafafanua.


### OFISA UTALII MKOA

Ofisa Maliasili wa Mkoa Ruvuma, Afrikanus Challe, anasema pori hilo lina kiwango cha juu cha hifadhi na inasimamiwa kisheria katika ulinzi, uendelezaji na matumizi ya busara ya mali hai, zikiwamo misitu, samaki na wanyamapori.

Utafiti umebaini kuwa pori Liparamba, ni eneo kipekee katika ukanda wa juu wa misitu ya miombo, ambalo lipo karibu na Ziwa Nyasa na uwapo wa msitu mpana wa asili na wenye mandhari ya kuvutia na eneo muhimu la kuhamia wanyamapori kati ya Tanzania na Msumbiji.

Anasema, serikali chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, imelenga kutenga eneo hilo pawe kielelezo cha ukanda wa viumbehai katika mazingira yao ya asili, kwa kupunguza kasi ya mabadiliko makubwa yatokanayo na uharibifu wa kibinadamu, itokanao na sababu mbalimbali.

Ni jambo ambalo sasa Challe anasema, ni sehemu ya utafiti wa mazingira, elimu ya uchunguzi wa miti, wanyama na samaki.





# Mradi uondoshaji mkubwa wa majitaka Dodoma kutekelezwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo mbioni kutekeleza mradi wa uondoshaji mkubwa wa maji taka katika Jiji la Dodoma.

Mradi huo utajumuisha ujenzi wa njia zenye urefu wa kilomita 250 za mabomba pamoja na mabwawa 16 yatakayojengwa katika eneo la Nzuguni.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprica Mahundi, aliyasema hayo jana jijini hapa alipozindua Baraza la Sita la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Dodoma (DUWASA).

Alisema lengo ni kuifanya Dodoma kuwa na sura ya makao makuu ya nchi.

Mahundi alisema ili mradi huo ufanikiwe kwa malengo yaliyokusudiwa, lazima wananchi wapatiwe elimu ya kutosha kwa kuwa ni wachache wanaofahamu kuwa wataunganishwa na mfumo huo kutoka kwenye makazi yao hadi kupeleka maji taka kwenye mabwawa.

Pamoja na hayo, aliitaka mamlaka hiyo kuongeza kasi ya utatuzi wa kero za wananchi ili kuleta tija katika mamlaka hiyo.

Alisema kero nyingine zimekuwa zikisababishwa na baadhi ya watu ambao wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakilalamika kutokana na huduma wanazozipata hivyo kupitia baraza hilo wahakikishe wanafanya kazi ya kuzitatua kero hizo ili wananchi wafurahie uwapo wa mtandao wa maji.

"Itoshe kusikia malalamiko hayo na ukiangalia wakati mwingine ni baadhi ya watu wanafanya kazi kwa mazoea, lakini tunahitaji kuona kwamba tunakuwa wabunifu na kujenga mtandao wa maji kuwa bora zaidi," alisema Mahundi.

Alisema kuna kila sababu ya DUWASA kuendelea kuujenga mtandao wa maji kwa kuwafikishia wananchi huduma za maji kwa kuwa wana uhitaji huo huku akisema wizara itaendelea kuiwezesha ili iweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Prof. Faustine Bee, alisema ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji Dodoma, wanaishawishi serikali na wadau wengine kuongeza kasi ya uwekezaji.

Prof. Bee alisema mamlaka peke yake haitaweza kuwekeza kwenye miradi mikubwa, ili kutatua tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika Jiji la Dodoma.

Alisema wanaendelea kuboresha huduma ya maji ili kuinua uwezo wa maeneo waliyopewa kuyasimamia hususani, Mpwapwa, Bahi na Chamwino na Kongwa kwa lengo la kuifanya mamlaka kuwa bora ndani ya Bara la Afrika

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph, alisema mamlaka imekuwa ikitekeleza mpango kwa muda mfupi wa kuchimba na kufufua visima zaidi ya 20 ili kukabiliana na tatizo ya maji Dodoma.

## TALIRI yataka wafugaji kutumia mifugo chotara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Kituo cha Mpwapwa, imewataka wafugaji kutumia teknolojia ya ufugaji wa kuchanganya mifugo ya asili na chotara, ili kubadilisha aina ya mifugo.

Hayo yalibainishwa jana na Mtafiti Msimamizi wa Idara ya Ng'ombe wa kituo hicho, Deogratius Masao, alipotoa ufafanuzi kuhusu utafiti wanaofanya kwa mifugo, ili kuhakikisha wafugaji wanabadilika.

Masao alisema teknolojia ya uzalishaji madume na kupandikiza kwa ng'ombe wa asili itasaidia wafugaji wengi kupata mifugo bora ambayo itakakuwa ikitoa maziwa mengi na nyama.

Alisema wao kama kituo cha utafiti, wamekuwa wakielimisha jamii ya wafugaji kuhakikisha wanatumia teknolojia hiyo ambayo itawasaidia kubadilisha ufugaji wanaofanya kadri siku zinavyokwenda.

"TALIRI Mpwapwa tunajitahidi kusambaza teknolojia hii kwa wafugaji, lengo letu ni kuona kila mfugaji ananufaika na teknolojia hii lakini pia kipato kinaongezeka," alisema Masao.

Alisema wafugaji wana kila sababu kufanya mabadiliko ya ufugaji wanaofanya hasa kipindi hiki ambacho taifa lipo katika uchumi wa kati, hivyo na wao wanapaswa kubadilika ili kuendana na hali ya sasa.

Mtafiti kutoka kituo hicho, Thomas Kabuni, alisema teknolojia ya kupandikiza mimba changa kwa ng'ombe jike itasaidia wafugaji kubadili aina ya ufugaji wanaofanya.

Pia, alisema wao kama watafiti, wamefanyia utafiti teknolojia na kuonyesha kuwa haina madhara na endapo itatumiwa na wafugaji, itawapa manufaa na kuwainua kiuchumi kutokana na kuwa mifugo bora yenye uhakika wa kutoa maziwa kwa wingi.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (kulia), akifafanua kuhusu kazi, muundo na majukumu ya wizara yake, mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, jijini Dodoma jana. Wa (pili kulia) ni Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Mary Makondo na Naibu Waziri wa Ardhi, Dk. Angelina Mabula. **PICHA: WIZARA YA ARDHI.**

# Msajili awapa siku 14 wafamasia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MSAJILI wa Baraza la Famasi, Elizabeth Shekalaghe, ametoa siku 14 kwa wafamasia wanaosimamia famasi ambazo hazipo katika maeneo yao ya kazi, kujisalimisha haraka kabla ya kuchukuliwa hatua kisheria.

Shekalaghe alitoa agizo hilo jana alipozungumza na maofisa habari wa Wizara ya Afya katika ofisi zake zilizoko katika Jengo la Bima ya Afya jijini hapa.

"Kwa wale wafamasia ambao wanasimamia famasi ambazo hazipo ndani ya maeneo yao ya kazi, ninatoa siku 14 kuanzia leo, kujisalimisha Baraza la Famasi, mtu anakaa Morogoro anasimamia famasi Dodoma, lakini taarifa alizotuletea sisi yupo Dodoma, sasa tumeshaanza kufanya ufuatiliaji maalum ili kuwabaini," alisema.

Shekalaghe alisema Baraza la Famasi limeanza kufanya ufuatiliaji maalum ili kuwabaini wafamasia wote wanaokiuka maadili na sheria kwa kutoa taarifa za uongo za kuonekana yupo kwenye kituo fulani wakati uhalisia anakuwa katika kituo kingine.

Alisema kifungu namba 43 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 kinaelekeza kwamba, hairuhusiwi mtu yeyote kujihusisha na biashara ya famasi kama siyo mfamasia, huku akisisitiza endapo mtu huyo atahitaji kufanya hivyo, atalazimika kutafuta mfamasia ili asimamie huduma hiyo.

Alisema Kanuni ya 10 ya Kanuni za Utendaji wa Taaluma za Mwaka 2020, zimeelekeza kwamba mfamasia atawajibika na usimamizi wa huduma katika famasi hiyo kila siku, huku akiweka wazi kuwa, kwa kiasi kikubwa bado wafamasia wengi hawawajibiki kwa kiwango cha kuridhisha katika maeneo yao ya kutolea huduma.

"Hivi karibuni kumekuwa na tabia ya wafamasia kuingia mikataba na wamiliki wa maduka ya famasi, huku wakishindwa kutekeleza majukumu yao, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni za utendaji wa taaluma na bado wakipokea mishahara ya usimamizi wa famasi hizo bila kufika na kutekeleza majukumu yao ya msingi," alisema.

Shekalaghe alitoa rai kwa wafamasia wote nchini kufika katika maeneo yao ya kazi.

## HABARI MBEYA

# Uzalishaji zao la soya kupanuliwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini, (TARI) Kituo cha Uyole, imeanza mpango wa kupanua kilimo cha zao la soya kwa kuandaa mbegu bora za kisasa.

Imesema lengo ni kuwasambazia wakulima kwa lengo la kukabiliana na udumavu kwa watoto na uhaba wa mafuta ya kupikia.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, wamekamilisha utafiti wa aina mpya za mbegu bora za soya na sasa wameingia hatua ya pili ya kuzalisha kwa wingi mbegu hizo ili kuanza kuwasambazia wakulima kwa lengo la kupanua kilimo cha soya nchini.

Dk. Bucheyeki alitoa kauli hiyo jana wakati wa akizungumza na waandishi wa habari juu ya maandalizi ya kupanda mbegu hizo katika msimu huu wa kilimo.

Alisema utafiti walioufanya unaonyesha mpango huo una faida kubwa kwa Watanzania kwani licha ya kukabiliana na tatizo la udumavu lakini pia utasaidia kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupika.

"Kituo chetu kimebuni aina nne za mbegu za soya ambazo zitapandwa kwenye kituo ili zianze kugawiwa kwa wakulima tunawasisitiza kuzingatia maelezo ya wataalam wa TARI ili wapate manufaa," alisema Dk. Bucheyeki.

Ofisa Uhawilishaji wa Utafiti wa Kilimo Kituo cha Uyole, Lusungu Paul, alisema kuwa wamekuwa wakisambaza teknolojia mbalimbali za kilimo kwa njia ya vipeperushi, Maonyesho ya Wakulima maarufu Nanenane na vyombo vya habari.


Aliongeza kuwa wakulima walio tayari kujifunza teknolojia za kilimo cha soya wafike katika ofisi za TARI Kituo cha Uyole au eneo la maonesho ya wakulima nane nane jijini Mbeya ambako tayari kuna mashamba darasa.

Mtafiti Mkuu na msimamizi mazao ya mikunde TARI Uyole, Michael Kilango, alisema wameamua kulima hekta nane za zao la soya.

Alisema waliamua kulima ukubwa huo ili kukidhi mahitaji ya wakulima kutoka maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Nyanda za juu kusini.

Meneja wa Shamba Kituo cha Uyole, Allan Mwanga, alisema wanatarajia kuazalisha zaidi ya tani 11 za mbegu za soya katika kituo.

Alisema baada ya kuzalisha mbegu hizo bora ambazo zimezingatia hatua zote za kitalaam na kuanza kuzisambaza kwa wakulima.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Twalibu Lubandamo (kushoto), akikabidhi pikipiki ya matairi matatu kwa Mwakilishi wa Kikundi cha Vijana Usafi Lugelele, Christian Joseph, mjini Rujewa juzi, ili itumike kwa ajili ya shughuli za uzoaji taka katika mji wa Igawa ikiwa ni mkopo kutoka Halmashauri. **PICHA: GRACE MWAKALINGA** .

# Makundi maalum Mbarali yapewa vifaa vya mil. 99/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali imekabidhi vitendea kazi mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 99 kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Vifaa hivyo ni matrekta, maguta na pikipiki ambavyo vimetokana na mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Twalibu Lubandamo, ndiye alikabidhi mikopo hiyo juzi kwa vikundi saba na kuwasisitiza wakopaji kulipa madeni yao kwa wakati ili na wengine wanufaike.

Alisema historia ya urejeshaji wa mikopo wilayani Mbarali ni wa kusuasua na kwamba licha ya kuendelea kutoa mikopo, lakini pia imeandaa mkakati wa kuvifuatilia vikundi vyote vilivyonufaika na mikopo hiyo kurejesha fedha.

"Vikundi vilikuwa ni vingi vilivyoomba mikopo, tumeanza na ninyi vikundi saba ambavyo tuliwanunulia vitendea kazi vyenye thamani ya Sh. milioni 99, tunaomba mmalize mkiwa mnafurahi ili msije baadae mkanuna kwa sababu kukopa sherehe kurudisha matanga," alisema Lubandamo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Daniel Kamwela, alisema, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020-2021 kiasi cha milioni 212 sawa na asilimia 10 ya mapato ya ndani kuanzia Julai hadi Desemba zilitolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa asilimia 100.

Kamwela aliongeza kuwa fedha hizo ziligawanywa kwa vikundi 5 vya wanawake vyenye wanufaika 91, vikundi 10 vya vijana vyenye wanufaika 132 pamoja na vikundi 4 vya watu wenye ulemavu vyenye wanufaika 24.

Ofisa Vijana wa Halmashauri hiyo, Christus Mwageni, aliongeza kuwa kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2020/2021 Halmashauri imefanikiwa kutoa Sh. 99,500,000 ambazo zimetumika kununulia matrekta ya mikono mawili ambayo yalitolewa kwa vikundi vya wanawake, matrekta matano ya mkono, pikipiki tano pamoja na guta moja ambavyo vyote vimetolewa kwa vikundi vya vijana vitano.

# RC awaagiza maofisa elimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa Mbeya, Albert Chalamila, amewaagiza maofisa elimu mkoani humo kuweka mazingira rafiki kwenye shule za msingi na sekondari yatakayowezesha upatikanaji wa elimu jumuishi.

Alitoa agizo hilo hivi karibuni wakati wa akizungumza na kamati ya Ushauri ya Mkoa, ambapo alisema hakuna haja ya kuwatenganisha watoto wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji kwani wote wanapaswa kujifunza pamoja.

Alisema mashirika mbalimbali yaliyojitolea kuhamasisha elimu jumuishi ni vyema yakaungwa mkono ili kuhakikisha watoto wenye uhitaji maalum wanapata elimu sawa na wengine.

Alisema Shirika la Child Support Tanzania CST, limefanikiwa kutoa elimu jumuishi kwa watoto bila ya kuwatenganisha likitumia mbinu za ubunifu ikiwamo ya kutumia vifaa vya kuchezea vinavyowafanya wanafunzi wenye uhitaji maalum wazingatie wakati mwalimu akiendelea kufundisha.

Alisema maofisa elimu katika Mkoa wa Mbeya wanapaswa kuiga mfano na kujifunza kutoka shirika la CST, na kwamba waachane na mfumo wa kuwabagua wanafunzi wenye uhitaji maalum mashuleni kwa kuwatenga kwenye shule zao au madarasa.

"Niwatake maofisa elimu na wengine mnaotusikiliza sasa katika shule zetu tuhakikishe tunaweza mazingira rafiki yatakayohakikisha watoto wetu kwa pamoja wanapata elimu jumuishi bila ya kuwatenganisha... nadhani wakati tulipotembelea lile darasa kuna kitu mmejifunza," alisema

Katika hatua nyingine, ameziagiza taasisi za umma na binafsi katika Mkoa wa Mbeya kuhakikisha zinatoa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu kwani nao wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi kama watu wengine.

Alitolea mfano hata ofisi yake ina watumishi wenye ulemavu na wanafanya kazi kwa bidii ukilinganisha na watu ambao hawana ulemavu wowote, huku akilipongeza shirika hilo kwa kuwa mfano wa kuwaajiri watumishi wake wenye mahitaji maalum.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa shirika la CST, Noela Msuya, ameiomba serikali kufikiria kuanza kutoa elimu ya Lugha ya alama kwa wanafunzi wa kuanzia darasa la awali ili miaka ijayo taifa lisiwe na uhaba wa walimu wa lugha hiyo.

"Jamii bado ina uelewa duni na mitazamo hasi kwa watu wenye ulemavu na jamii jumuishi nadhani ni kitu ambacho tunapaswa kuendelea kukipazia sauti ili watu wengi zaidi waelewe lakini pia serikali itusaidie kuihamaisha jamii ishiriki kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki zao za msingi katika jamii," alisema.



# ZIPA yaagizwa kurekebisha miundombinu ya uwekezaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), imetakiwa kurekebisha mazingira ya miundombinu ya barabara katika maeneo ya uwekezaji.

Wito huo umeutolewa na Mwenyekiti wa muda wa Kamati ya Uchumi na fedha ya Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alipozungumza na watendaji wa Mamlaka hiyo, Maruhubi, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema Zanzibar uchumi wake unategemea zaidi uwekezaji iwe wa viwanda au uwekezaji katika sekta binafsi na iwapo yatawekezwa na sekta ya huduma itaingia kati.

Alisema kuwa kuna maeneo huru yamewekezwa kwa muda mrefu, lakini kuna kero kwa wawekezaji katika huduma za barabara ambazo haziridhishi.

"Kwa mfano Fumba barabara imejengwa na serikali, lakini bado haipo vizuri mpaka inafikia wawekezaji kutaka kuingiza gharama zao wakati ZIPA walijizatiti kuweka maeneo hayo kwa kuweka barabara pamoja na maji kabisa, ili kumfanya mwekezaji akija awekeze moja kwa moja na sio kushughulikia hayo," alisema.

Alisema Zanzibar ni visiwa viwili vya Unguja na Pemba, lakini bado katika kisiwa cha Pemba ZIPA inahitaji kufanya kazi ya ziada ili kuimarisha uwekezaji.

Alisema kutokana na uwekezaji kulala kisiwani kunasababisha vijana wengi wa Pemba kuondoka na kukimbilia Unguja kutafuta maisha na kukuta hata maeneo ya kilimo kuvamiwa na makazi ya watu.

"Lakini ZIPA kama mngekuwa mmejitahidi kutengeneza mazuri zaidi na tunashukuru kauli ya mheshimiwa rais aliyoitoa hivi karibuni ya kuweka mazingira maalumu kwa ajili ya Pemba nafikiri ndugu zetu wangekuwa hawapati tabu tena hakuna mtu anayependa kuhama kwao bali wanafuata maisha," alisema.

Alitaka kujua ZIPA wamejipanga vipi kwa ajili hiyo.

Akizungumzia suala la miundombinu ya barabara, Mkurugenzi Rasilimali watu na Fedha, Vuai Yahya Lada, alisema suala la kuweka miundombinu ni la serikali, lakini wanajitahidi kuhakikisha yanakuwa bora.

Hata hivyo, alisema hadi kufikia Desemba 31, mwaka jana, jumla ya miradi 760 imeshaidhinishwa na mingi yao ni ya utalii ambayo yamefikia kwa asilimia 60 na mtaji zaidi ya Sh. bilioni saba.

Alisema miradi hiyo imetoa ajira za moja kwa moja 50,000.



Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana (kulia), akizungumza na wafanyabiashara wa samaki katika Soka la Malindi, mjini Unguja jana. **PICHA: HAWA ABDALLAH**.

# Waajiri wanaowapa wafanyakazi likizo za corona kuchukuliwa hatua

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema haitosita kuwachukuliwa hatua waajiri ambao bado wanaendelea kuwapa likizo bila ya malipo wafanyakazi wao kwa kisingizio cha maradhi ya corona.

Agizo hilo limetolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, ofisini kwake Mwanakwerekwe alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu muundo wa ajira hasa katika kipindi hiki cha ajira.

Alisema serikali ilitoa toleo namba moja la 2021 la kuwaagiza waajiri kusitisha likizo hizo, na kuwarejesha kazini ndani ya mwezi huu, lakini bado wanaendelea kuwapa wafanyakazi wao likizo bila ya malipo na wengine kuwapa mishahara pungufu mpaka kipindi hiki ambacho biashara imeimarika vyema.

Aliwatahadharisha waajiri wa aina hiyo kuwa serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaoenda kinyume na sheria za nchi na maelekezo ya serikali.

"Ni imani yangu kwamba waajiri wote wataitikia wito na kutekeleza ipasavyo maelekezo ya serikali ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika kukuza na kuzilinda ajira za staha zilizopo," alisema.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), lilitangaza uwapo wa maradhi ya corona duniani hatua iliyosababisha nchi nyingi ikiwamo Zanzibar kuchukua tahadhari ikiwamo kudhibiti uingiaji wa wageni.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali ya biashara ya utalii kuimarika, wizara yake haioni uhalali wowote wa waajiri kuendelea kutoa likizo bila ya malipo ambazo zilitolewa kwa sababu ya janga la corona kwa wafanyakazi wao baada ya mwezi wa Desemba.

Alisema ni mategemeo ya serikali kuwa wafanyakazi wote watarudi kazini na kuanza kazi ndani ya mwezi huu.

# Wafanyabiashara wa samaki waombwa ustahimilivu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, amewataka wafanyabiashara wa soko la samaki lililopo Malindi na madalali wa mnada wa eneo hilo kuwa wastahimilivu wakati uongozi wa mkoa ukiwatafutia ufumbuzi wa kudumu matatizo yao.

Idrissa alitoa wito huo jana wakati alipofanya ziara katika soko la Malindi na mnada wa samaki kufuatia maombi ya wafanyabiashara hao kurejeshewa mnada katika soko hilo na kutolewa njia kwenye uzio wa mabati ya ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la Malindi.

Alisema serikali ya mkoa itafuatilia kwa karibu matatizo yao ili kubaini sababu ya kusita kwa muda mrefu ujenzi wa soko la kisasa la samaki Malindi ambalo limesitisha shughuli za wafanyabiashara hao.

"Naomba tuendelee kufanya subira wakati viongozi wenu tukifuatilia tatizo lenu ili kuona nini kimesababisha kusita kwa mradi huu ambao kukwama kwake umezuia shughuli zenu kwa muda sasa," alisema Idrissa.

Alisema atashirikiana na wizara inayoshughulikia masuala ya uvuvi ili kuona tatizo linalowakabili wafanyabiashara hao linapatiwa ufumbuzi wa haraka ili wafanye kazi zao na kujiongezea kipato kama ilivyokuwa hapo awali.

"Nipeni muda matatizo yenu hayana majibu ya haraka, nitakuja na waziri anayeshughulikia masuala ya uvuvi atusaidie kupata majibu ya mustakabali wa soko jipya, kwanini limekaa muda bila ya kuendelea ujenzi," alisema.

Mapema wafanyabiashara hao wameuomba uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kurejesha mnada katika eneo hilo pamoja na kuwatolea njia itakayowarahisishia kufika katika eneo la mnada huo badala ya kutumia mzunguko kubwa kutoka Malindi hadi Msikiti Mabluu huku wakiwa na mizigo.

"Mkuu wa Mkoa tumekuwa tukifanya kazi zetu katika mazingira magumu kwasisi wa soko hili kama haujarejeshwa mnada hatuna biashara tunalala tu hapa, wenzetu wa mnada wa samaki wanatembea pwani kwa pwani kutoka Malindi hadi katika mnada Bwawani Msikiti Mabluu ni mbali mno ikizingatiwa wana mizigo ya samaki mikononi na wengine kichwani," walisema wafanyabiashara hao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG. PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)
Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 184/2020

Ombi la JIMBA ABDALLA KUNGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu **ABDALLA HAMISI KUNGA.**

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/01/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 28/12/2020.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATH
I (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;22/2021

Ombi la RACHEL OSWARD SIMULE, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **WILFRED PETER MUNGATTA.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **23/02/2021** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **21/01/2021.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)
Katika mahakama ya mwanzo CHAMWINO MJINI
Usimamizi wa mirathi 04/2021

Ombi la STERE ONASAA MUSHI kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu PENDO JACOB MUSHI.

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **29/01/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 21/01/2021.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO… OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late DAVID KASIAN MSOLA**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by MARTHA EZEKIEL IDABU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 17 Day of 2 /2021
Dated at Dodoma this 20 day of 01/ 2021

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GODFRID LAISERY MREMA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya Honda yenye namba za usajili **T 330 BJK**, Yenye chassis namba **LSYPCJLO8A0284311** na Injini namba **156FM1ACO52135**

Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**MOS/TR/RB/132/2021**

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA

# Rais Biden aahidi demokrasia, ushirikiano, heshima, utu



Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel (Kushoto), akimpongeza Makamu wa Rais Marekani, Kamala Harris. **PICHA: ALLIANCE**

**WASHINGTON,** Marekani

JOE Biden (78), ameapishwa kuwa rais wa 46 wa Marekani, akimrithi mtangulizi wake, Donald Trump ambaye hata hivyo hakushiriki sherehe za uapisho.

Kutoshiriki Trump wakati Biden akiapishwa, ni kurejewa tukio la kihistoria lililowahi kutokea takribani miaka 152 iliyopita, nchini humo.

Biden alikula kiapo hicho, juzi, ikiwa ni utaratibu wa kikatiba nchini humo, kuiongoza Marekani kwa kipindi cha miaka minne, mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu, John Roberts.

Sherehe za kuapishwa Rais Biden pamoja na Makamu wake, Kamala Harris, zilifanyika eneo la Capitol, jijini Washington majira ya mchana kwa nchini Marekani, ikiwa majira ya saa mbili usiku, Afrika Mashariki. Licha ya sherehe hizo kuhudhuriwa na watu wachache kutokana na corona, viongozi maarufu walishiriki wakiwamo marais wastaafu.

Rais George W. Bush alihudhuria, pia Bill Clinton na mkewe Hillary Clinton na Barack Obama na mke wake Michelle Obama, ni miongoni mwao.

**HOTUBA YA KWANZA**

Biden, akizungumza baada sherehe hizo, alisema Trump, alimuandikia barua na kuiita ya faragha, asingependa kuisoma hadharani, ingawa hadi akiapishwa Trump hakuwahi kumpongeza kwa ushindi wake.

Biden alisema Marekani imefanya mengi ikiwamo kusimamia demokrasia, kutokana na kufanya mabadiliko ya nafasi za kisiasa ikiwamo urais kwa amani takribani karne mbili.

"Demokrasia imeshinda, leo tunasherekea sababu demokrasia imeshinda, sherehe yetu wote, hapa tuliposimama pana zaidi ya miaka 100, nani atasema Marekani hakijafanya chochote ni historia kuwa na mwanamke makamu wa rais.

Msiseme hatujabadilika kwa zaidi ya karne."

"Janga hili ni changamoto, virusi (corona) vimewachukua wengi. Ni wakati wa kuwa pamoja, hatuwahi kufeli. Tuanze kusikilizana mmoja baada ya mwingine, kuheshimiana, kila mmoja," alisema Biden baada ya kuapa ikiwa ni hotuba yake ya kwanza akiwa rais.

Hotuba ya Biden aliyoitoa jana kwa dakika takribani 30, aliendelea kusisitiza kulinda demokrasia, umoja na amani huku akisema nguvu ya pamoja itamuondoa adui corona.

"Kila mtu anahitaji heshima, kuheshimiana, Marekani tunahitaji kurudisha nguvu na heshima ya Dunia kwa kushirikiana," alisema Biden.

Rais Biden alieleza kuwa Marekani imefanya mabadiliko na maendeleo na kuendeleza taifa kubakia lenye nguvu kubwa duniani, licha ya sasa kukabiliwa na virusi vya corona. Biden, aliwataka wahudhuriaji wa sherehe hizo kusimama kimya kwa dakika ili kuwakumbuka Wamarekani waliopoteza maisha kutokana na kutetea taifa pamoja na watu 400,000 waliofariki kwa corona.

Rais huyu anaweka historia ya kuwa rais wa kwanza kufanya kazi kwa karibu zaidi na waafrika, ofisini.

Katika kipindi cha rais wa nchi hiyo wa awamu ya 44 iliyoongozwa na mwafrika, Barack Obama, Biden alikuwa makamu wake wa rais. Hivi sasa Biden akiwa rais, makamu wake, Kamala Harris ni mwafrika.

**MUUMINI MZURI**

Rais Joe Biden, kabla ya kufika kula kiapo Cha kiti Cha urais, alihudhuria misa katika Kanisa Kuu lililopo Washington, akiwa pamoja na viongozi wanne wa Baraza Kuu la Katoliki, ambao pia ni wanatoka vyama tofauti, chama chake yaani Democratic na Republican.

**SIKU YA KWANZA OFISINI**

Katika siku yake ya kwanza ofisini, Rais Biden, alianza kazi kwa kutengua sera kadhaa muhimu za Trump na kusaini maagizo ya watendaji 15 kukabiliana na kusambaa kwa virusi vya corona.

Pia alibadilisha msimamo wa utawala wa Trump kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na suala la wahamiaji.

Biden akiwa katika ofisi ya rais, Oval, Washington, baada ya kuapishwa, katika hotuba yake alisema atafanya kazi na Wamarekani wote, bila kujali itikadi huku akiahidi ushirikiano mpya kutoka Marekani mpya, chini yake.

"Marekani iko nyuma yenu. Marekani lazima ithibitishie ulimwengu kuwa imejiandaa kuongoza tena, sio kwa mfano tu wa nguvu, bali kwa nguvu za mfano wetu," alisema Biden, akiwa katika ofisi ya rais, maarufu Oval Office.

"Nitafanya kazi na Wamarekani wote, hata ambao hawakuniunga mkono wakati wa kugombea," alisema Biden.

**MATARAJIO KIMATAIFA**

Biden katika siku za mwanzo katika ofisi yake ni matarajio ya kuboresha Marekani katika ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi na nchi nyingine.

Pia, Biden katika baadhi ambayo anasema ataanza nayo ni kwamba, atairejesha Marekani katika Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi, ambao unatarajiwa kuanza kwa kutekelezwa nchini humo, Februari, 19, mwaka huu.

Utekelezaji wa mkataba huo ni kwa mujibu wa Ibara namba 21 kipengele(3) na Marekani ilijiunga na mkataba huo, Aprili, 22 mwaka 2016 na kuelezea nia yake ya kuanza kuutekeleza tarehe 3 Septemba mwaka 2016.

Marekani, wakati wa utawala wa Trump, ilijiondoa kwenye mkataba huo, Novemba 4, mwaka jana. Baada ya kauli hiyo, jana, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, mjini New York, alitoa taarifa ya kufarahishwa Marekani kurudi kwenye mkataba huo.

Gutteres, alisema anaipongeza Marekani kwa hatua ya rais mpya, Joe Biden kuirejesha Marekani katika Mkataba wa Paris Mabadiliko ya Tabianchi.

**AFRIKA ITARAJIE NINI?**

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa, wanaeleza, kipindi cha miaka minne ya utawala wa Donald Trump na kauli yake mbiu ya 'Marekani kwanza' haikulitilia maanani hata bara la Afrika.

Pia, Trump, mara chache aliwahi kutoa maneno na kuzikashifu nchi za Kiafrika akitumia lugha mbaya na kupuuzia wito kumtaka aombe radhi.

Kuja kwa Rais Biden, kunatajwa na wachambuzi hao kwamba huenda atarudisha misimamo ya watangulizi wake, ambao walibadili sura ya uhusiano na Afrika

Kipindi ambacho, uhusiano uliimarika Kati ya Marekani na Afrika kiuchumi, ni baada ya kumalizika vita baridi, wakati wa utawala za Bill Clinton, George W.Bush na Barack Obama.

Ajenda ya marais hawa kuhusu Afrika ilipata uungaji mkono kutoka vyama vyote na mabaraza yote mawili ya bunge la Marekani, wawakilishi na Seneti.

Wakati wa utawala wa Clinton biashara ya Afrika chini ya mpango wa African Growth and Opportunity Act (AGOA) wa mwaka 2000 ambao uligeuka sheria, ulirefushwa na Bush pamoja na Obama.

Mpango huo, umerefushwa hadi mwaka 2025, huku mkataba huo ukiyafungulia mataifa ya Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara, soko la biashara nchini Marekani.

Masharti ya mpango huo, ilikuwa nchi husika zihakikishe zinapiga hatua kuboresha demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu.

Mwaka, 2003, Bush alizindua mpango wa msaada wa dharura wa kupambana na UKIMWI (Emergency for Aids Relief) huku Obama, akienga Dola bilioni nane kwa mwaka, kulisaidia bara la Afrika.

Bush, Clinton na Obama, mwaka 2013, walikutana nchini Tanzania, wakati wa ziara ya Obama, tukio ambalo liliweka historia ya marais wawili wa zamani wa Marekani na mwenzao aliyekuwa madarakani, kukutana katika nchi moja kwa wakati mmoja.

**BIDEN NI NANI?**

Rais Biden, ni mwanasiasa was siku nyingi ambaye mwaka 1972 alichaguliwa kuwa seneta lakini hata kabla hajaanza kutumikia kiti hicho, alipata pigo baada ya mke wake wa kwanza na binti yake kufariki katika ajali ya gari.

Aliwahi kuwania nafasi ya urais nchini humo mara tatu, lakini hakufanikiwa.

Biden alishinda kwa kura milioni 73, dhidi mshindani wake Trump akipata kura milioni 70 kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Novemba 3, mwaka jana, anakuwa rais mwenye umri mkubwa kuwahi kutokea katika historia ya Marekani, rekodi hiyo awali ilishikiliwa na Trump ambaye ana miaka 74.

***Makala hii imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao.**



# ZIDANE: HAKUNA AIBU MADRID KUFUNGWA

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesisitiza hakuna aibu kwa Real Madrid kufungwa na timu ya daraja la chini ya Alcoyano kwenye mchezo wa kombe la Copa del Rey.

Madrid ilitolewa kwenye hatua ya 32 wakati Juanan alipofunga bao la ushindi dakika ya 115, Jumatano.

Jose Solbes awali alisawazisha bao la mapema la Eder Militao na Alcoyano ikapata ushindi licha ya kumpoteza Ramon Lopez kwa kadi nyekundu wakati wa muda wa ziada. Lakini kocha mkuu wa Madrid, Zidane alikanusha madai kwamba kipigo hicho ilikuwa ni aibu kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

"Hayo ni maneno yenu. Maneno yenu, hayanihusu mimi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Huu ni mchezo wa soka, mambo nu magumu kwa sababu tulicheza dhidi ya timu ya daraja la chini na mara zote tunataka kushinda mechi, lakini mwisho wa siku mambo hayakuwa kama tulivyotarajia na hiyo haimaanishi kuwa ni aibu.

"Inaweza kutokea na inatokea wakati mwingine kwenye soka na tunatakiwa kukukubaliana na hali halisi. Nimeshamaliza kufanya hivyo.

"Tutaendelea kujituma kwa bidii... siku nyingine ya maumivu kwa sababu hatutaki kupoteza tena."

# Klopp hajui Van Dijk anarudi lini dimbani

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ametoa maendeleo ya majeruhi Virgil van Dijk, lakini bado hana uhakika mlinzi wake huyo ni lini atarudi uwanjani kuwachezea mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England.

Van Dijk alifanyiwa upasuaji wa goti Oktoba baada ya kuumia goti kwenye mchezo wa 'dabi' ya Merseyside dhidi ya Everton.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amekuwa nje ya Liverpool kwa muda mrefu ambapo sasa wapo nafasi ya nne kwenye msimamo ikipitwa pointi sita na vinara Manchester United.

Klopp ameelezea maendeleo mazuri kuhusu Van Dijk, lakini hana uhakika lini mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 29 atarudi uwanjani.

"Kwa uhakika anaonekana vizuri," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilizungumza naye asubui hii kwa simu (juzi), kwa hakika yupo kwenye hali nzuri na inaonesha kwamba anaendelea vizuri, lakini sijui lini atarudi uwanjani.

"Kwa uhakika kabisa bado anatakiwa kuendelea kutibiwa. Hata mimi nilishawahi kupata maumivu kama hayo."

Tangu Van Dijk kuanza kucheza kwenye Ligi Kuu akiichezea Liverpool Januari mwaka 2018, vijana hao wa Klopp walishinda mechi 72 kati ya 95 wakiwa nae.







# *Majeruhi ya De Bruyne yamtia hofu Guardiola*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaamini Kevin De Bruyne anaweza akawa ameumia nyama za paja wakati wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Aston Villa, ingawa bado anasubiria taarifa zaidi.

De Bruyne alitolewa kipindi cha pili wakati City wakiwachapa Villa na kuwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi.

De Bruyne alitolewa nje kabla ya Bernardo Silva na Ilkay Gundogan kufunga ndani ya dakika 11 za mwisho nyumbani kwa Villa, na kuibuka na ushindi huo.

Kyle Walker pia aliumia dakika ya 28 ya mchezo huo na Guardiola alipoulizwa kuhusu mawili hao alisema.

"Kwanza sijazungumza na daktari." "Kyle aliniomba nimtoe nje kwa sababu kitu fulani kilitokea.

"Kevin alishika mguu wake kwa mkono. Pengine litakuwa tatizo la nyama za paja. Lakini nini unatarajia?

"Ni kawaida, wakati mwingine vitu hivi vinatokea kwa aina ya mchezo wenyewe."

City sasa haijafungwa katika mechi 16 za mashindano yote.

HABARI MICHEZO

# Garcia kutua Barca Juni

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itamsajili, Eric Garcia kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu, mgombea wa urais wa klabu hiyo, Toni Freixa amesema.

Mlinzi huyo wa kati amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Camp Nou, ambako alicheza katika timu ya vijana hadi mwaka 2017, kwani aliiambia City mwaka jana hatasaini mkataba mpya.

Ilionekana wazi kwamba, Barca wangeweza kumrudisha Garcia mwezi huu kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi, lakini Freixa amebainisha kwamba, ni ngumu kufanya usajili Januari hii kutokana na matatizo yao.

Badala yake, nyota huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 20 anatarajia kiujiunga na klabu hiyo mara mkataba wake utakapomalizika mwaka huu.

Akizungumza baada ya kukutana na bodi ya muda ya Barca, Freixa alinukuliwa na Sport akisema: "Tumeshatoa thamani ya usajili wa Eric Garcia, lakini atakuja hapa kipindi cha majira ya joto wakati msimu unaelekea mwisho na atakuwa huru."

Freixa, ambaye anagombea urais dhidi ya Joan Laporta anayepewa nafasi kubwa na Victor Font, amesema kocha mkuu Ronald Koeman hajatoa mapendekezo yoyote hadi sasa.

Jambo lililo wazi ni kwamba, Barcelona hawataweza kufanya usajili wa fedha nyingi kutokana na soka la duniani kuathirika na mlipuko wa virusi vya corona.







# MARTINEZ KUMALIZANA NA INTER

**MILAN,** Italia

INTER Milan ina matumaini makubwa ya kufikia makubaliano ya kumpa mkataba mpya, Lautaro Martinez, kwa mujibu wa Sky Sport.

Majaliwa ya nyota huyo wa Inter, Lautaro Martinez yamekuwa yakipamba zaidi vyombo vya habari, huku uvumi ukidai kwamba, anaweza kuondoka klabuni hapo.

Baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia pale Inter, Martinez mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda Barcelona.

Mkataba wa sasa wa raia huyo wa Argentina na Inter unamalizika mwaka 2023, lakini sasa mambo yanaonekana yanaweza kubadilika.

Kwa mujibu wa ripoti ya Sky Sport jana Alhamisi, wakala wa Martinez alikutana na uongozi wa Inter Jumatano.

Martinez amefunga mabao tisa katika mechi 18 za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu, huku pia alikuwa amefunga mabao 14 katika mechi 35 kwenye Ligi msimu wa 2019-20.

# *Pirlo afurahia kubeba taji kama kocha*

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Juventus, Andrea Pirlo, amesema kubeba taji lake lake la kwanza kama kocha ni "wakati mzuri zaidi" kuliko hata mafanikio aliyoyapata wakati akicheza.

Mabao kutoka kwa Cristiano Ronaldo na Alvaro Morata katika vipindi vyote viwili, yaliwawezesha Juve kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Napoli na kushinda kombe la Supercoppa, Jumatano.

Kwenye mchezo huo nyota wa Napoli, Lorenzo Insigne akikosa penalti na hivyo kuwapa urahisi Juve kulibeba taji lake la kwanza msimu huu.

Pirlo alishinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya na Kombe la Dunia katika kipindi chake cha uchezaji, lakini alisema amejisikia fahari zaidi kulibeba taji hilo akiwa kocha.

"Ni furaha kubwa," alisema Pirlo, ambaye alichukua nafasi ya Maurizio Sarri mwanzoni mwa msimu huu, akiiambia Rai Sport. "Kubeba taji la kwanza kama kocha ni kitu fulani tofauti, nzuri zaidi kuliko nilipokuwa mchezaji.

"Nipo kwenye tanuru la timu muhimu, katika timu ya kihistoria."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA: NAFURAHIA KUFUNGA BAO ZURI

●●● Kama hupigi, huwezi kujua nini nitatokea, nina furaha kubwa mpira ulikwenda ndani...

**LONDON,** England

PAUL Pogba ataendelea kucheza kwa tabasamu usoni mwake ikiwa tu Manchester United inaendelea kushinda, ameelezea baada ya kufunga bao la ushindi kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England.

**United ilipata ushindi wa 2-1 dhidi ya Fulham Jumatano, ikirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu mbele ya Leicester City na Manchester City ambazo zilishinda dhidi ya Chelsea na Aston Villa.**

Kikosi hicho cha kocha Ole Gunnar Solskjaer kiliruhusu bao kwa mara ya kwanza katika mechi saba za ugenini na Pogba akafunga la ushindi baada ya lile la Edinson Cavani la ufunguzi kusawazishwa na Ademola Lookman.

Pogba alifunga bao hilo kwa jitihada binafsi kwa kutumia mguu wa wake wa kushoto ikiwa ni mara ya kwanza tangu Januari 2015 wakati alipokuwa bado yupo Juventus.

Lilikuwa bao ambalo kiungo huyo alilielezea kuwa ni nzuri na akaiambia BT Sport: "Nilipiga vizuri. Sikutegemea mguu wa kushoto kama utakuwa na nguvu namna ile, lakini tunatakiwa kujaribu.

"Kama hupigi, huwezi kujua nini nitatokea. Kwa hakika nina furaha kubwa mpira ulikwenda ndani.

"Lilikuwa bao zuri na ushindi mzuri - hilo ndio jambo la muhimu zaidi."

Bao hilo lilikuwa la pili kwa Pogba mwenzi huu kuwapa ushindi United, pia akifunga bao pekee dhidi ya Burnley.

Bado pia alikosa nafasi kubwa za kufunga dhidi ya Aston Villa na Liverpool tangu kuanza kwa mwaka huu 2021, ambapo kwa kushindwa kwake kufunga pale Anfield Jumapili iliyopita, kuliwafanya United wakose pointi mbili.

Alielezea baada ya kufunga bao la ushindi juzi, Pogba alisema: "Sio kama naomba radhi, lakini kwa uhakika nilikuwa kama kichaa; nilikuwa kichachaa haswa, kwani nilikuwa karibu na goli na pengine ningefanya kitu bora zaidi.

"Leo mambo yamekwenda tofauti, hivyo nina furaha kwa hilo. Jambo la msingi ni kwamba tulipata ushindi leo (juzi), kwa sababu ulikuwa mchezo mgumu."

## ZISIKUPITE

### YAMTAKA ODEGAARD

ARSENAL inataka kujaribu kumsajili kiungo wa Real Madrid na Norway, Martin Odegaard, 22. ***(Sky Sports)***

### ROWE MKATABA MPYA

ARSENAL imempa ofa ya mkataba mpya mchezaji wake kiungo, Emile Smith Rowe, 20, ambao sasa atapata mshahara wa pauni 40,000 kwa wiki. ***(Mail)***

### LINGARD AGOMBEWA

TOTTENHAM Hotspur, West Ham na Sheffield United ni miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili kwa mkopo kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard, 28. ***(Talksport)***

### PSG KUMSAJILI GARCIA

PARIS St-Germain inapanga kufanya usajili wa kushangaza kwa mlinzi wa kati wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia, 20. ***(Mundo Deportivo)***

### CHELSE NA KOCHA

CHELSEA inapanga kutafuta kocha wa muda kuchukua nafasi ya Frank Lampard ambaye amekalia kuti kavu. ***(Independent)***

### IHEANACHO AWANIWA LEIPZIP

KELECHI Iheanacho, 24, wa Leicester City, Divock Origi, 25, wa Liverpool na fowadi wa Nice, Kasper Dolberg, 23, wapo kwenye orodha ya washambuliaji wanaotakiwa na RB Leipzig. ***(Bild)***

### DANNY ROSE HUYO UTURUKI

MLINZI wa kushoto wa Tottenham Hotspur na England, Danny Rose, 30, anatakiwa na klabu ya Trabzonspor ya nchini Uturuki. Nyota huyo mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### TOMORI AKARIBIA MILAN

KLABU ya AC Milan inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Chelsea, Fikayo Tomori, 23. ***(Gazzetta dello Sport)***

### EN-NESYRI HUYO WEST HAM

WEST Ham inaandaa ofa mpya yenye thamani ya pauni milioni 32 kwa ajili ya straika wa Sevilla na Morocco, Youssef En-Nesyri, 23. ***(Star)***

### WOLVES KUCMHUKUA JOSE

KLABU ya Wolves inakaribia kumnasa kwa mkopo straika wa Real Sociedad, Willian Jose, 29, huku kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja. ***(Telegraph)***

### VERON AWANIWA MAN

MANCHESTER United inawania kumsajili fowadi wa Palmeiras na Brazil, Gabriel Veron, 18. ***(Sport - via Star)***

# HABARI MICHEZO

## Azam warejea kupambana kwenye Ligi

**Na Saada Akida**

BAADA ya siku 10 za kambi ya Visiwani Zanzibar, Kikosi cha Azam FC kinarejea leo jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya maandalizi ya raundi ya 19 ya mzunguko wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati alisema kambi huyo imewasaidia kujenga ubora wa kikosi cha timu hiyo kuelekea duru la pili la ligi hiyo.

Alisema ratiba walikuwanayo imekuwa ya siku 10 za kambi na mechi 3 za kirafiki na mechi ya juzi, ndo ilikuwa ya tatu na wamemaliza ratiba za kukaa Zanzibar

"Kuhusu siku 10 za kambi hapa Zanzibar tumejaaliwa kujenga timu kwenye kila sehemu na maandalizi yamekuwa mazuri sana kiwango tulichokihitaji kinaonekana," alisema.

Alisema wanaporejea Dar es Salaam wataendelea na mazoezi kuhakikisha wanafikia malengo ya msimu huu wakiwa na lengo la kutwaa ubingwa wa Ligi hiyo.

Azam baada ya kuondolewa katika hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Mapinduzi, kikosi hicho kilibaki Zanzibar kwa ajili ya kambi.

## TFF kuwanoa viongozi klabuni

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Shirikisho la Soka la Tanzania, (TFF), umeaanda semina ya viongozi wa Klabu kwa ajili ya kuimarisha utawala bora katika klabu za soka nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko, Boniface Wambura, alisema semina hiyo itakuwa kwenye mikoa miwili Arusha, Morogoro pamoja na Visiwani Zanzibar.

Alisema huo ni mpango mkakati wa TFF kwa miaka minne ya Rais Walence Karia kutoa elimu kwa viongozi wa klabu kwa ajili ya utawala bora.

Alisema Semina ya kwanza itakuwa ya utawala bora ambayo itafanyika Januari 24, 2021, katika sehemu hizo mbili kwa kutolewa na wataalamu ambao inawahusisha Wenyeviti wa klabu za soka pamoja Zanzibar ikishirikiana na viongozi wa Shirikisho hilo (ZFF).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi Tanzania, ( TPLB), Karim Boimanda kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara, itaendelea kwa mechi za mzunguko wa 19 ambazo zitacheza kuanzia Februari 13, mwaka huu.

# ADOLF ATOA NENO KWA TAIFA STARS CHAN

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa Taifa Stars, ambaye kwa sasa ni kocha, Mohamed Rishard 'Adolf', amesema kuwa haoni tatizo lolote kwa timu ya taifa kuchaguliwa au kupangwa hata wachezaji tisa kutoka klabu moja.

**Adolf alisema hayo akieleza tathimi ya mechi ya Stars dhidi ya Zambia, ambapo ilifungwa mabao 2-0, Jumamosi nchini Cameroon kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani, CHAN.**

Alionyesha kushangazwa na Tanzania kunyanyaswa na timu ya taifa ya Zambia kwa miaka ya karibuni, wakati enzi zao miaka ya 1980, ilikuwa haifui dafu kwao.

"Wakati tunacheza na Zambia haijawahi kutufunga hata siku moja. Kwa sababu tulikuwa tunaweza na wao hawatuwezi. Siku hizi Zambia wanatuweza na sisi hatuwawezi," alisema Adolf.



Kocha huyo (pichani) wa zamani wa Prisons, alisema uteuzi wa kikosi usiwe wa kisiasa zaidi, badala yake uangalie zaidi uwezo wa wachezaji kiasi kwamba, hata kama wakichaguliwa saba au tisa kutoka klabu moja isiwe tatizo.

"Tuwe na wachezaji saba wanatoka timu moja au tisa sawa tu, ili mradi awe na uwezo, lakini pia hao ni Watanzania kama wana uwezo wa kutuwakilisha wacheze tu," alisema.

Mimi nimeshawahi kuichezea Stars ambayo tulikuwa wachezaji wa tisa wa Pan African, lakini ndiyo kikosi hicho kilichofuzu kwa mara ya kwanza AFCON mwaka 1980," alisema Adolf ambaye ndiye alifunga bao pekee nchini Tanzania mwaka 1979 dhidi ya Zambia lililosababisha Stars kufuzu AFCON baada ya kutoka sare ya bao 1-1 mechi iliyofuata nchini Zambia, bao la kusawazisha likifungwa na Peter Tino.



Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen (katikati,) akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na tamasha la Sauti za Busara kwa mwaka huu, na kueleza kuwa jukwaa hilo ni fursa kwa Watanzania na Afrika kwa ujumla katika kutangaza utamaduni wa Afrika Kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

# JKU wajipanga kuiadabisha Black Sailor

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya JKU, Omar Khamis "Kocha Matu" amesema amejipanga vyema kuwakabili Black Sailor kwa kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu katika mchezo wa Ligi Kuu Visiwani Zanzibar.

Ligi Kuu ya Zanzibar inatarajiwa kuendelea kesho Jumamosi, baada ya kusimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi, iliyomalizika wiki iliyopita na Yanga kulibeba taji hilo.

Kesho michezo mitatu itapigwa kwenye viwanja tofauti, ambapo JKU watawaalika Black Sailor, huku Hard Rock itacheza na Malindi na Mafunzo watakipiga na Chuoni.

Akizungumza na gazeti hili kuelekea mchezo wake huo, Omar alisema kuwa wachezaji wake wapo vizuri na hakuna mchezaji wa kikosi cha kwanza ambaye ataukosa mchezo huo, hivyo anaamini atapata ushindi utakaompa nafasi ya kujiweka sehemu salama zaidi katika msimamo wa ligi kuu ya Zanzibar.

"Mchezo utakuwa mgumu kutokana na timu zimepata muda kwa wachezaji wao kupumzika hivyo kila timu itahitaji kupata ushindi na sisi tumejiandaa kupata ushindi, Black Sailor ni timu nzuri na naiheshimu inawachezaji wadogo na vijana ambao wanakasi ya kucheza mpira,"alisema .

Kesho michezo mitatu itapigwa kwenye viwanja tofauti, ambapo JKU watawaalika Black Sailor, huku Hard Rock itacheza na Malindi na Mafunzo watakipiga na Chuoni.

Ligi hiyo ambayo kila timu tayari imeshacheza michezo nane, inaelekea ukingoni mwa mzunguko wa kwanza kabla ya kuanza mzunguko wa lala salama.

Timu ya JKU katika msimu huu imeanza vibaya baada ya kuambulia vipigo vitatu, sare tatu pamoja na kupata ushindi michezo miwili kati ya michezo nane waliyocheza na kuifanya timu hiyo kuwa katika nafasi ya 10 katika msimamo, ikiwa na alama 9 huku Black Sailor wakiwa nafasi ya pili na alama 14.

# Michezo

Ijumaa Januari 22, 2021
Nipashe




Pogba: Nafurahia kufunga bao zuri UKURASA 22

# Mwambusi ajiweka kando Yanga SC

## ● ● ● Matatizo ya kichwa ndio sababu, Msolla afafanua atakayeziba nafasi yake na...

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Klabu ya Yanga, Juma Mwambusi (pichani), ameomba kukaa kando kwa muda ndani ya kikosi cha timu hiyo, kwa sababu anasumbuliwa na maumivu ya kichwa kwa muda mrefu sasa.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwambusi alisema amekuwa akisumbuliwa na jino kwa muda mrefu na kupata maumivu makali ya kichwa.**

Na amekuwa akitumia dawa bila ya kupata nafuu, hivyo akalazimika kurudi Hospitali ya taifa ya Muhimbili, ambako ameshauriwa kufanyiwa upasuaji mdogo.

Alisema anatarajiwa kufanyiwa operesheni ndogo Jumatatu ya Januari 25, mwaka huu, kwa ajili ya kutenganisha mshipa mdogo na jino.

“Baada ya vipimo iligundulika kwamba, nina matatizo katika mfumo wa meno, mshipa wa kichwa umeungana na jino, ndio imeleta tatizo kubwa na jopo la daktari limenishauri nipumzike kidogo na kazi kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji mdogo, kutenganisha mshipa huo na jino,” alisema Mwambusi.

“Jumatatu natarajiwa kufanyiwa upasuaji huo mdogo, hivyo sitaweza kujihusisha na timu, endapo nitashauriwa kuachana kabisa na soka basi nitalazimika kukaa pembeni na kufanya shughuli zingine,” aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema wamepokea barua ya Mwambusi ya kuomba kujiweka kando na kutaja sababu ni matatizo ya kiafya.

Kuhusu kutajwa kwa kocha wa Afrika Lyon, Nizar Khalifani kuchukua nafasi ya Mwambusi, Msolla alisema bado hawajaamua lolote kwa sasa, kwa sababu jukumu hilo wamemuachia Kocha Mkuu, Cedric Kaze.

“Tunasubiri Kocha Kaze akihitaji kutafutiwa basi tuna wachezaji wengi waliopita Yanga ambao ni walimu, kama atamtafuta mwenyewe tupo tayari au kuamua kubaki na kocha wa makipa hilo mikononi mwake,” alisema Msola.



Mwambusi amekuwa kocha msaidizi wa Yanga kwa vipindi viwili tofauti akiwa chini ya Hans Van Puljim raia wa Uholanzi na sasa chini ya Kaze raia wa Burundi, huku pia akihudumu kama kocha Mkuu wa Mbeya City kwa nyakati mbili tofauti.




Bruno Fernandes (katikati) wa Manchester United, akikabwa na mabeki wa Fulham, wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya England baina ya timu hizo uliofanyika Jumatano. Man United ilishinda 2-0. **PICHA: MTANDANO**

# Simba wajifua, kocha kutangazwa

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Simba kinaanza mazoezi kesho Jumamosi kujiandaa na hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku jina la Kocha Mkuu likitarajia kutangazwa wakati wowote.

Mratibu na klabu hiyo, Abbas Ally, amesema kuwa baada ya kuwapa mapumziko ya siku nane wachezaji wao, wanatarajia kuanza rasmi mazoezi Jumamosi kwa wale ambao hawako kwenye kikosi cha timu ya Taifa.

“Kuna wachezaji ambao walisafiri kwenda kwao nje ya nchi na hata ndani ya nchi, wapo pia ambao walikuwa hapa hapa Dar es Salaam. Wote, kasoro waliopo kwenye timu ya taifa ya Tanzania, wanatakiwa kuanza mazoezi Jumamosi kwa ajili ya kujiandaa na Ligi ya Mabingwa na mechi za Ligi Kuu,” alisema mratibu huyo.

Kuhusu kocha, alisema klabu inaweza kumtangaza wakati wowote kuanzia kesho, ambaye atakuja kujumuika na kikosi kwa ajili ya maandalizi ya michuano hiyo.

“Kuanzia Jumamosi anaweza kutangazwa Kocha Mkuu na atakuja kuungana na wachezaji waliopo. Kumbuka kuwa makocha wapo wengi sana, lakini klabu kubwa kama Simba siyo ya kusumbuka kupata makocha, kila kitu kinakwenda vizuri na atatangazwa,” aliongeza.

Klabu ya Simba iliwapa mapumziko wa siku nane wachezaji wake mara baada ya michuano ya Kombe la Mapinduzi ilipofungwa kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya wapinzani wao wa jadi Yanga, baada ya suluhu ya bila kufungana kwa dakika 90.

Kwa sasa pia Simba haina Kocha Mkuu, baada ya Sven Vandenbroeck kuikacha timu hiyo na kwenda kujiunga na AS FAR ya Morocco.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042